# *Utambulisho*

Mnaweza kuketi. Asante sana, ndugu, Ndugu Shores. Ni . . . Hakika ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa usiku wa leo, katika . . . hii First Assembly of God, tena, kushirikiana kwenye Neno la Mungu, nanyi watu wazuri, kuwa pamoja na mpendwa wetu Ndugu Shores tena, na—na ndugu wote ambao tumekutana kote katika juma. Na tumekuwa na wakati mzuri sana, wiki hizi mbili zilizopita.

2 Sijui kama nimewahi, kwa miaka, kuwa na wakati mzuri zaidi kuliko nilivyokuwa nao wiki hii, ya kushirikiana na ndugu karibu kote katika Bonde hili la Maricopa, kote kutoka Mesa, chini, na chini hadi Tucson, ambayo ni Yerusalemu, kwa kweli, kwenye kilima. Na tuna furaha kutembelea pamoja na ndugu zetu hapa Yeriko, unaona, hapa chini huko . . . huko chini ya kilima. Nilishangaa tu kwamba hiyo itakuwaje.

3 Na kwa hivyo nilipokuwa hapa, miaka mingi iliyopita, huo kila wakati ulikuwa ni ushindani kati ya Tucson na Phoenix. Kwa hivyo, niliwazia tu hiyo hivi majuzi, unajua. Walikuwa wakinitania kuhusu kuitetea Tucson. Na kwa hivyo niliwazia, vema, ni juu ya kilima, na Yeriko iko bondeni, mwajua. Kwa hivyo nilidhani hiyo itakuwa nzuri tu. Vema, tunamkamata Bw. Katikati basi, mwingine anakuja chini. Tunataka kumfanyia kazi.

4 Sasa, umekuwa wakati mzuri, kama ninarudia, na hakika tumejifurahisha sana.

5 Sasa, sisi tunashu- . . . tukingojea kwa hamu kubwa mkutano huu ujao kuanzia kesho usiku. Tunatarajia wakati mzuri. Na katika hili nimejaribu kuweka, kwa njia yangu nyenyekevu ya kuifanya, msingi, kidogo nilete mwamko kati ya watu, kwa ajili ya uamsho unaokuja. Na sasa tuna wahubiri wazuri wanaokuja, katika uamsho huu ulio karibu sasa. Ndugu Velmer Gardner, na—na ndugu fulani wa Kimethodisti anayepaswa kuwa mhubiri mashuhuri, na halafu, kwa hilo hitimisho kuu la mwisho kabisa, ni Ndugu yetu wa thamani Oral Roberts, kwa ajili ya Jumatatu ijayo usiku. Na nina imani kwamba Mungu atawapa ndugu zetu jumbe ambazo zitafanya Phoenix kupiga magoti, kutetemeka, kwa hofu ya Mungu.

6 Nasi tulijaribu sana, wiki hii, ku—kuweka msingi kwa ajili ya hiyo, ya kuonekana kwa Mwana wa Mungu hivi karibuni. Nami ninaamini, na nimekuwa nikifundisha, kwamba inawezekana kabisa kwamba angeweza kuja katika kizazi hiki sasa, hata usiku huu. Hatujui itakuwa lini, lakini tunataka kuwa tayari sana hivi kwamba, wakati utakapokuja, tutaenda pamoja na Yeye katika Unyakuo.

7 Imekuwa wakati mzuri. Nimekuwa nikihubiri Jumbe hizi nzito juu ya Kuja Kwake, na kujaribu kuweka u—uwezekano, na saa ambayo tunaishi sasa, na jinsi ambavyo kila kitu, kwa maoni yangu, maoni yangu manyenyekevu, kiko katika hali tu ya Kuja kwa Bwana, Unyakuo, jambo linalofuata. Na yote ambayo hayapo, yanaweza kutokea ndani ya saa moja.

8 Ninaamini, wengi, sijui tu ni wangapi, lakini unabii kadhaa mashuhuri unaohusu kutimia kwa kuja kwa Masihi na kile Yeye angefanya, kilitimizwa katika saa saba za mwisho pale msalabani. "Jinsi walivyochoma ubavu Wangu, na ninii Yangu. . .hakuna mfupa uliovunjika." Na—na Yeye akalia, "Mungu wangu, mbona umeniacha?" Na unabii mkuu, ulitokea tu, moja, mbili, tatu, nne, hivyo tu, ndani ya saa moja au mbili tu, mbalimbali.

9 Sasa, hiyo inaweza kutokea vivyo hivyo wakati wa kurudi Kwake. Nasi lazima tuwe macho, tukingojea.

10 Jana jioni nilifikiri tulikuwa na wakati mzuri huko chini kwenye—kwenye Assembly of God kusini mwa hapa. Ninaamini ni Kusini, labda, inaitwa, Assembly ya Kusini. Nilikutana na ndugu mzuri ambaye sikuwa nimewahi kukutana naye hapo mbeleni katika safari, kama ninavyokumbuka, lakini ndugu wa thamani na kikundi kizuri cha watu.

11 Nasi tukazungumza, hapo jana usiku, juu ya Ujumbe wa. . . wa kuwa na Yeye kama mahali penye rutuba na maji jangwani, mahali, kumkumbuka Yeye, yale yote aliyokuwa amefanya, tulipokusanyika pamoja, tukikaa katika sehemu za Mbinguni katika Kristo. Na kukumbuka mambo ambayo Yeye alifanya, na mambo ambayo Yeye aliahidi kufanya, jinsi alivyoahidi atakutana nasi. "Popote pale walipokusanyika wawili au watatu katika Jina Lake, kwamba Yeye angekuwa hapo kati yetu." Halafu, nilifikiri ukuu wa Mungu ulionyeshwa vizuri sana wakati Yeye alipokuja chini moja kwa moja kati yetu, na kujithibitisha Mwenyewe, kwamba Yeye alikuwa hapo pamoja nasi tena. Hiyo inafanya tu kuwa isiyo na ujinga, kwamba tuko karibu na mwisho. Na mambo hayo Yeye aliyoahidi kufanya, mwisho kabisa, na tunaona yanatukabili sasa.

12 Nadhani, labda, kwamba watu wengi hapa ni—ni watu waliookoka. Na sisi ndio tunaomba na tunajitahidi sasa kwa mkutano ujao. Na lazima tujikaze pamoja na yote yaliyo ndani yetu, na tufanye kila tuwezalo. Tuhakikishe kwamba tunazungumza na kila mwenye dhambi wakati wa mkutano huu. Tumwendee kila mfanyabiashara, na kila mtu ambaye hajaokoka, na wale wasio na Kristo, bila Roho Mtakatifu. Tunataka kuwaendea kwa Ujumbe, kwa njia thabiti ya Injili, yenye busara, ya kuwaendea watu.

13 Acha maisha yetu yakolee chumvi sana, hata wengine wanaweza kutazama jinsi tunavyotenda na kuishi, hata

watataka kuishi hivyo, pia. Mnajua Yesu alisema, "Ninyi ndio chumvi ya dunia." Lakini ikiwa chumvi imepoteza ushuhuda wake, la—ladha yake, nguvu yake ya kuvutia, basi haiwezi tena kuponya wala kuokoa. Chumvi huokoa wakati inapogusa, na lazima sisi—lazima sisi tuwe mguso wa Mungu. Sisi ndio mahali Pake pa kugusia, kama Ndugu Roberts mara nyingi huzungumzia kuweka mkono wake kwenye redio au kitu fulani kama mahali pa kugusanishia.

14 Sasa, huenda ukanisikia nikizungumza kigeni kidogo usiku wa leo, lakini siku tatu au nne usiku zilizopita nimelazimika kuchukua sauti yangu ya juu. Mimi—mimi. . . Ile nyingine imechoka. Kwa hivyo, nazungumza juu juu, zaidi sana kutoka juu ya kinywa changu. Sio kujifanya, bali inanibidi kufanya hivyo, ili kuzuia sehemu ya chini isiumie. Unajua, Mungu hutuumba kwa njia fulani, ambapo, ikiwa sehemu moja imechoka, tunaweza kukamata nyingine. Mtu—mtu. . . Unajua, akiba.

15 Na mtu fulani aliniuliza, fulani, wakati mmoja, akasema, "Unawezaje kutembea kwa bidii kupitia milima na kadhalika?"

16 Nikasema, "Vema, nilijifunza hiyo, mbinu kidogo, miaka mingi iliyopita, kutoka kwa Wahindi." Unaona? Unaweza kutembea na magoti yako, usitumie sana, nyonga yako, na kuacha nyonga zako zipumzike. Kisha utembee na nyonga yako, na kupiga hatua, na kuacha magoti yako yapumzike, unaona. Kwa hivyo kupumzika tu na kutembea, kupumzika na kutembea, kupumzika na kutembea.

17 Hivyo ndivyo unavyohubiri, na ya juu kisha ya chini, ya juu na ya chini. Unaacha moja ipumzishe, nyingine.

18 Loo, Mungu alifanya jambo la ajabu alipomwumba mwanadamu! Unajua ni kwa nini? Ilikuwa ni katika mfano Wake ambao Yeye alimwumba mwanadamu. Na kwa hivyo ni nini kingine kingeweza kuwa cha ajabu zaidi ya Mungu?

19 Nimekuwa nikihubiri sana juu ya—juu ya Kuja kwa Kristo katika wakati huu, nilifikiria labda itakuwa jambo zuri usiku wa leo kutulia juu ya baadhi ya mambo haya ambayo nimekuwa nikiongea juu yake, na kuleta u—uzito wa hali ya siku hii, mbele yetu, kwa Injili, na kuona jinsi sisi wenyewe tulivyoandaliwa, kwa ajili ya saa hii. Tunajuaje? Huu unaweza ukawa ndio mkutano wa mwisho ambao Wafanyabiashara hawa watakuwa nao. Unajua, huu unaweza kuwa usiku wa mwisho ambao First Assembly of God na makanisa mengine yote nchini kote yatakuwa yamefunguliwa. Kesho, inaweza kutokea, yote yamefungwa. Hatujui. Huenda hii ikawa ndiyo mara ya mwisho kusoma Biblia kwa kusanyiko hili. Kwa hivyo, acha kwa namna fulani tujichunguze usiku wa leo na tuone mahali tulipo, kwa uzito, kwa muda kidogo.

20 Na kisha tutaenda, tujaribu kumaliza mapema, ili tuweze kuachilia watu watoke na sio kuwashikilia. Nilitoa tamshi lisilofaa wiki hii, kwamba mimi—mimi huwaweka muda mrefu wakati wa usiku, ikiwa najua kukosa kazi ya siku moja, hiyo haitawaumiza. Lakini nikasema, "Jumamosi usiku sasa, siwezi kuwaweka muda mrefu hata kidogo, kwa sababu hamwezi kukosa shule ya Jumapili. Lazima muwe pale kwenye wajibu wenu." Kwa hivyo, sasa, sitawaweka muda mrefu usiku wa leo, maana bila shaka ninawatakeni hapo kesho usiku. Hiyo ndiyo tumekuwa tukiendeshea gari, wakati huu mzuri.

21 Na sasa waombee wale ndugu wote ambao watazungumza. Omba kwamba Mungu atawatia mafuta wajumbe Wake. Na usiku huo wa mwisho, na Ndugu Oral; amechaguliwa kwa ajili ya kuhitimisha kabisa hayo yote. Ninawaza juu ya wakati huo wa mwisho, kama ilivyokuwa siku ya mwisho ya sikukuu wakati Yesu alisimama na kulia kwenye hekalu. Lo, naomba tuisikie tena. Mungu na atulilie, na atuite kwa upande Wake, wakusanyike katika Kanisa, wakombolewa Wake, Bibi-arusi Wake ambaye kwa neema amemnunua kwa Damu Yake Mwenyewe. Nasi tunaombea mwisho huo.

22 Sasa tunaenda kumtazamia Bwana sasa hivi katika maombi kabla hatujakaribia Neno Lake. Kwa sababu, mnajua, Neno si la kutafsiriwa apendavyo mtu binafsi, kwa hivyo napenda tu Mwandishi alifunue; na kujitenga na Hilo, mnajua, ili kwamba tu tuweze—tunaweza kuamini kwamba Yeye anafanya hivyo. Kwa hivyo hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa hivi. Na—na tunapoinamisha vichwa vyetu, hebu tuinamishe mioyo yetu pia, tuinamishe tu mioyo yetu kwa Mungu.

23 Sasa tukiwa tumeinamisha vichwa na mioyo yetu, je, kuna haja moyoni mwako usiku wa leo, raia mwenzangu wa Ufalme, ndugu yangu msafiri? Wewe ambaye unasafiri hapa Phoenix na maeneo mengine, kwamba tumekusanyika katika kanisa hili dogo la kupendeza usiku wa leo kumwabudu Yeye, je, kuna haja ambayo ungependa Mungu aijue? Ishikilie akilini mwako, na uinue tu mkono wako, na useme, "Bwana, acha iwe mimi sasa usiku wa leo. Ni—nina hi—hitaji kubwa." Naomba Yeye . . . Najua Yeye ataiona. Ataisikia. Ataijibu.

24 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukaribia Wewe kwa imani sasa. Tunajiunga pamoja, tukiweka maombi yetu kama mtu mmoja. Kwa imani tunaondoka hapa, kwenye barabara ya 11 na Garfield, na tunapanda juu kwa imani, kupita mwezi na nyota, juu kwenye Njia Nyeupe ya Kilimia, huko ndani na kupita mapazia ya dunia hii, hadi kwenye Uwepo wa Mungu. Na hapo juu ya Madhabahu ambapo Dhabihu imewekwa, na Makerubi na Maserafi wanaruka juu ya Madhabahu ya Mungu, wakilia, "Mtakatifu!" Loo, ni mahali pa jinsi gani kusimama! Lakini kwa Neno hili lililoandikwa, na Mwana wa Mungu, kwamba, "Tukimwomba Baba chochote kwa Jina Lake, atatupatia."

Na hapo Yeye ameketi na mavazi Yake yaliyolowa Damu. Gharama imeishalipwa, ili sisi, tusiostahili, tuweze kumkaribia Yeye, kama wana na binti, baada ya kumpokea Kristo kama Mwokozi wetu.

25 Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, usiku wa leo, kwanza, kutusamehe uovu wetu, na yote ambayo tumefanya na kusema, ambayo hayakuwa sawa tu machoni Pako. Na, Mungu, tunajua hayo ni mambo yasiyohesabika ambayo tumefanya. Turehemu, Mungu, kwa kuwa hatuyazungumzi tu mambo haya ili kusikika, lakini sisi tu—tunazungumza mambo haya kwa—kwa upendo, na kwa uchaji, na kwa imani kwamba Mungu atatusikia na kujibu maombi yetu kwa ajili ya wengine na sisi wenyewe. Unajua kilichokuwa nyuma ya kila mkono, lengo na nia.

26 Bwana, yatandaze mabawa Yako makubwa matakatifu, tuseme, usiku wa leo. Na Uwepo Wako uliotukuka uhisiwe sana miongoni mwetu, usiku wa leo, hata tutaogopa. Mungu, tunataka kujua mahali petu tu pa kusimama sasa. Tunakagua, kuchukua hesabu ya maisha yetu. Huenda ikawa ni kabla tu ya Unyakuo, wito wa kuondoka.

27 Na tunatarajia mkutano huu ujao huko Ramada kesho usiku, na tunataka kuchunguza maisha yetu wenyewe usiku wa leo na kuona ni wapi tumepungukiwa, ili tuwe vyombo katika mkono Wako, udongo uliofinyangwa na kuumbwa na Mungu wa Mbinguni, ili tuweze kutarajia katika tukio hili kuu ambalo litatimia, tunayoitoa si kwa sababu yoyote nyingine ila kwa ajili ya Ufalme na utukufu wa Mungu. Bariki juhudi zetu dhaifu za juma hili, Bwana, kujaribu kuchochea, miongoni mwa watu, utambuzi wa saa tunayoishi.

28 Ongea nasi usiku wa leo, kupitia kusomwa kwa Neno, na hebu Wewe uchukue maandishi na—na kufunua muktadha kwa njia ambayo Roho Mtakatifu angependa tuijue. Na sifa zote zitakuwa Zako. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

29 Watu wengi wanapenda kuandika maandishi, na kufikiria nyakati wangependa kuyarejelea. Na mara nyingi, wahudumu, kama nifanyavyo, mimi mwenyewe, sisi—sisi huweka maandishi wakati mwingine, kuyarejea. Mhudumu fulani alizungumza juu yake, na sisi . . . Wazo fulani dogo lilishika akili zetu. Na tunapenda kulirejelea, wakati mwingine, kusema, "Vema, hiyo ni . . . Niliona kitu walipokuwa wakilisema." Hiyo ni sawa.

30 Sasa, tunataka kusoma usiku wa leo, katika Biblia, kutoka kwenye kitabu cha barua ya Wafilipi, Paulo akiwaandikia Wafilipi, katika sura ya 2, 5 hadi 8. Tungependa kusoma haya kwa ajili ya fungu, wakati ukisoma nasi, au kutupa usikivu wako usiogawanyika tunapojitahidi kulisoma.

31 Sasa, wakati mnapofungua mahali hapo kwenye Maandiko, ningependa kusema kwamba nimepewa mimi, ndugu yenu, majaliwa ya kuzungumza Jumapili hii ijayo alasiri kwenye

mkutano. Ilikuwa nia yangu kuwapo sasa wiki nzima, na kuketi mahali fulani kwenye hadhira, au mahali pengine, kusikiliza na kujaza na kulisha nafsi yangu mwenyewe kwa Neno la Mungu, kama vile ndugu zetu watakavyoileta, na shuhuda za wafanyabiashara. Na ninatumaini kuwaona ninyi nyote kule. Mkutano ni wakati wa alasiri, kwa hivyo makanisa yatafungwa, kote. Wewe, utakaribishwa zaidi kuja. Tunakutarajia wewe, huo na kila mkutano mwingine.

32 Sasa katika Wafilipi 2:5, tunasoma.

> *Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu, ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu:*
>
> *Ambaye, mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho:*
>
> *Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu:*
>
> *Tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*

33 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake. Ningependa kuchukua, kwa dakika chache za wakati wenu, juu ya kile ningekiita, au ningependa kusema, somo linaloitwa: *Utambulisho*. Kutambua, kutambuliwa kwa kufanana na wahusika wa Biblia! Kutambuliwa kwa kufanana na wahusika wa Biblia! Na usiku wa leo, kama nilivyofikiria, katika kuliendea hili, baada ya kuwa wiki hii tumekuwa tukiongea juu ya Kuja Kwake, na jinsi ambavyo Kanisa linapaswa kujiweka tayari.

34 Leo nilipokuwa nimeketi chumbani, nilikuwa na jambo fulani moyoni mwangu ambalo nilitaka kuzungumza leo usiku, "Dhabihu kuu." Lakini, ilionekana, Roho Mtakatifu alionekana kunisogeza pembeni kutoka hapo, kwenda kwenye njia nyingine ya kufikiria. Wahudumu wote wanajua hiyo ni nini. Wewe, unafikiri una kitu unachotaka kusema, na halafu, ghafla, unajisikia kwamba unapaswa kusema kitu kingine, labda kinyume. Labda ni kwa ajili ya mtu mmoja tu. Sijui. Lakini, mimi nina umri mkubwa wa kutosha katika Kristo, kujua kufuata mwongozo wa Roho. Kile Roho anachosema fanya, kifanye.

35 Nina hakika usiku wa leo kwamba tunapaswa kujikuta mahali fulani katika mhusika fulani wa Biblia, ili tuweze kujua matokeo ya mhusika huyo na kujua matokeo yetu yatakuwa nini.

36 Inanikumbusha hadithi ndogo niliyosikia wakati mmoja, ya mwa—mwanamke fulani, alikuwa amemleta mvulana wake mdogo kutoka—kutoka mashambani mahali fulani, ambako

waliishi, akamleta mjini, ku—kumtembelea bibi yake. Na mvulana huyo mdogo, akiishi nyuma . . .

37 Katika sehemu yangu ya nchi, huko Kentucky, *mashambani* inamaanisha katika nyumba ya magogo mahali fulani, na vibao vya zamani vya kuezekea juu yake. Na kwa hivyo kioo chetu, nyumbani, kilikuwa kipande cha kioo kilichobandikwa kwenye mti, ambapo, nje, ambapo kuna benchi ndogo ya kufulia iliyojengwa juu ya mti, na pampu ya gudulia, ambapo baba angevuta maji na kunawa mikono yake, na kipande cha kioo hapo. Nami nimemuona Mama akisimama nje hapo na kuchana nywele zake, maana hakukuwa na kioo ndani ya nyumba.

38 Mvulana huyu mdogo lazima alilelewa katika nyumba kama hiyo. Na aliposhuka kumtembelea bibi yake, alikuwa na m—mlango ambao, upande wake wa nyuma, ulikuwa kioo. Na mvulana huyo mdogo kwa namna fulani alikuwa mpweke. Na alikuwa akiangalia pande zote za nyumba. Na baada ya kitambo kidogo, ilitokea kwamba aliangalia kupitia mlangoni. Nao ulikuwa umefungwa, tangu walipoingia. Na—na kwenye kioo ubavuni mwake, alimuona mvulana mdogo. Akaanza kwenda kwa yule mvulana mdogo, kufanya urafiki naye. Na alipoanza kuchungulia kwenye kioo hiki, alisogea karibu. Na akageuka, akasema, "Mbona, mama, huyo ni mimi."

39 Na hicho ndicho tunataka kuangalia usiku wa leo. Ninataka kujiangalia mimi, na ninataka ujiangalie mwenyewe. Na tunapoangalia kwenye Kioo kikubwa cha Mungu cha Neno Lake, hebu ninii yetu . . . kuweza kujitambulisha na wengine ambao tutazungumza juu yao, wahusika wengine wa nyakati zingine. Na ninataka kujiona niko ndani—ndani ya kioo cha Mungu cha kujitazama. Maana, ikiwa chochote kitakuonyesha mahali umesimama, ni Kitabu *hiki*. Hakuna kitabu kama Hicho, kwa sababu Hicho chote ni Ukweli. Sisemi kwamba vitabu vingine si vya kweli, lakini mimi—mimi najua Hiki ni kweli. Yote ni Ukweli, kwa sababu ni Neno la Mungu.

40 Sasa, Yesu alitupa Mfano wa kile tunachopaswa kuangalia, wakati alipodhihirisha Maisha Yake kwetu kupitia Neno, kile tunachopaswa kuona. Tunapoangalia kwenye kioo cha Mungu, tunapaswa kujiona tukitambulishwa Naye. Huo ni Mfano kamili.

41 Sasa, lakini tunaona kwamba, tunapoendelea na maisha, kwamba tabia yetu huumba sura tuliyo nayo. Kila mmoja anajua hilo. Wewe, unavyoishi, ndivyo tabia yako ilivyo, hukuumba kuwa kile ulicho. Sasa, umeona watu ambao unapenda tu kuwa karibu nao, ingawa huenda wasiwe katika—katika kitengo chako cha jamii. Na, tena, wanaweza kuwa wa jamii tofauti, weusi, au wa kahawia, au wa manjano. Lakini kuna kitu tu kuhusu mtu huyo, hata unapenda tu kuwa karibu nao. Kwa

sababu kila mtu ni da—dainamo ndogo yao wenyewe, na wewe—wewe unaweka mazingira.

42 Na halafu unaona watu ambao walikuwa watu wazuri, lakini hata hivyo daima ulifurahia kukaa mbali nao. Ni kwamba tu wa—wanaunda mazingira kama haya mahali ulipo. Hakuna chochote dhidi yao, wao ni watu wazuri, lakini hupendi tu mazingira hayo, wao, wao ni . . . wako ndani. Na tabia yao huunda chochote walicho, huwafanya walicho.

43 Wakati Mungu alipoangalia kiumbe Chake kilichopotea, baada ya kukibuni na kukifanya kama vile Yeye alivyokitaka . . . Na mimi—mimi ninapenda kukiangalia katika asili yake. Mimi—mimi ninapenda mambo ya nje, kwa sababu, hapo, hicho lazima kiwe vile anavyokitaka Yeye, la sivyo asingekifanya hivyo. Na tunakuja karibu na kukipotosha, na kutengeneza kitu kutoka kwacho ambacho hakimpendezi. Lakini, tabia Yake ya upendo, imeumbika; Mungu, akiona kwamba ninii Yake—kwamba mpango Wake mkuu na uumbaji wa wanadamu kuishi duniani, na kuishi kwa amani, na kutokufa kamwe, asiwe mgonjwa wala kuwa na huzuni au wasiwasi wowote. Loo, ni—ni njia ya jinsi gani ambayo Baba alitupatia! Na hiyo ilikuwa ninii Yake—hiyo ilikuwa mapenzi Yake, pia, sisi kuwa katika njia hiyo. Hakutaka tuwe katika hali ya kufa kama tulivyo. Hii, na ha—hali ambayo ulimwengu uko leo, kamwe sio mapenzi ya Mungu. Hakukusudia hivyo, hata kidogo.

44 Lakini alipoona kwamba kiumbe Chake kilikuwa—kilikuwa kimeanguka, sasa tabia Yake mwenyewe ya upendo ilimwumba Mwenyewe ndani ya Utu wa Kristo. Tabia ya Mungu Mwenyewe ya upendo ilimdhihirisha Mwenyewe ndani ya Mtu, Kristo. Wakati Paulo akizungumza hapa, "Akifikiria sio unyang'anyi, bali anajifanya Mwenyewe sawa, sawa na Mungu, hasa." Unaona? Tabia yake Mwenyewe ilimuumba Mtu wa aina hiyo. Loo, hakuna mtu angaliweza kufanya hivyo isipokuwa Mungu. Hii ilifanywa ili aweze kulipa adhabu ya kuanguka kwa kiumbe Chake. Unaona? Yeye . . .

45 Lazima kuwe na kitu cha kukiokoa kiumbe hiki. Na hakuna kitu kingeweza kukiokoa, kwa sababu kiumbe cha juu zaidi cha uumbaji Wake kilikuwa kimeanguka, na kila kitu chini yake kilianguka pamoja nacho, kwa sababu kilianguka. Kuna kitu kimoja tu kilichobaki, ambacho hakikuanguka, na hicho kilikuwa ni Mungu, mbingu. Kwa hivyo kitu cha mbinguni kilibidi kishuke kukomboa kiumbe hiki, kwa sababu hakukuwa na kitu hapa ambacho kingeweza kukiumba. Na upendo wa Mungu mwenyewe kwa ulimwengu uliumba tabia iliyoonyeshwa katika Kristo. Alikuwa tabia ya Mungu. Alikuwa sura ya Mungu iliyodhihirishwa. Ndani Yake kulikuwa na Mungu, Mungu ndani ya Kristo, akijifunua Mwenyewe kwa ulimwengu. Na hakuna upendo unaoweza kuwa mkubwa kuliko upendo huo,

kwamba, Mtu kama huyo angekuwa kile alichofanya Yeye, ili—ili kukomboa kile kilichokuwa kimepotea.

46 Hiyo inapaswa, wazo hilo tu hapo hapo, linapaswa kuitia aibu Phoenix na ulimwengu wote, kuona ni hali gani ambayo tumeangukia. Na kile...Mungu, akijidhihirisha Mwenyewe, kufanya mpango wa ukombozi, ku—kukomboa hii tabia yetu iliyoanguka.

47 Hii ilifanywa ili adhabu iweze kulipwa, kwa sababu a—adhabu ilikuwa kifo. Na mmoja chini ya hukumu ya kifo hakuweza kulipa adhabu ya yule mwingine chini ya hukumu ya kifo. Kwa hivyo ilibidi kuwe na Mtu ambaye alikuwa huru kutokana na kifo, ili alipe adhabu. Na hakuna mwingine ambaye angekuja isipokuwa Mungu, kwa sababu alikuwa Ndiye pekee ambaye alikuwa huru kutokana na adhabu ya mauti.

48 Sasa, kwa hivyo, tabia Yake ya upendo ya kupenda, loo, kwetu sisi, hiyo—hiyo inafanya dhahiri Yohana 3:16. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele." Mungu, akijidhihirisha Mwenyewe, na kuwa Mwanadamu, ili juu Yake aweze kuwa na umbo la kiumbe Chake. Kwa maneno mengine, alibadilisha hema Yake. Aliitandaza miongoni mwa wanadamu.

49 Na mtoto mchanga, Yehova, akilia katika hori, unaweza kuwazia hilo? Inapaswa kuiwasha moto mioyo ya waaminio. Na hayo yote yalifanyika...Je, unaweza kuwazia, Yehova akiwa mtoto mchanga katika—katika hori, katika—katika zizi la samadi? Je, unaweza kuwazia hayo? Unaweza kuwazia, mtoto Yehova akicheza kama—kama mvulana? Ni mfano. Je, unaweza kuwazia, Yeye akiwa tineja? Je, unaweza kuwazia, Yeye katika karakana ya seremala? Na unaweza kuwazia, Yeye katika utii mkamilifu kwa Mungu, akifa msalabani, kukomboa kiumbe Chake kilichoanguka? Hiyo ndiyo aina ya upendo ambao Mungu alikuwa nao. Na ilibidi awe huyo, ili afe, aushike uchungu wa kifo.

50 Sasa, ninaamini, siku chache zilizopita usiku tulikuwa tunaelezea jambo fulani kwa utaratibu huo, alipokuja. Na Yeye alituma manabii na watu mashuhuri, na Yeye alimtuma Musa na manabii, na akatoa sheria. Lakini hawa wote hawangeweza kukomboa, kwa sababu walikuwa bado wanadamu chini ya adhabu ya kifo. Wala hawakuweza kulipa adhabu ya kifo, ingawa walikuwa vibao vya kuelekezea ambavyo vilielekeza kwa Yule mkamilifu ajaye, kwa sababu hawakuwa wakamilifu. Lakini wakati Huyu alipozaliwa, alizaliwa bila dhambi.

51 Mungu, Yehova, alimtia uvuli bikira na akaumba seli ya Damu. Na wakati Huyo alipozaliwa, alikuwa ni Mwana wa Mungu. Kwa maneno mengine, ilikuwa maskani. Ilikuwa mahali

pa kuishi ambapo Yehova angeweza kuishi miongoni mwa watu Wake na kujidhihirisha Mwenyewe, kile alichokuwa.

52 Ni mfano jinsi gani, jinsi Mungu mtakatifu alivyojidhihirisha, halafu akachukua nafasi ya mtumishi, kutawadha miguu! Na kusema, kwamba, "Ndege wana viota, na—na mbweha wana pango, bali sina mahali pa kulaza kichwa Changu." Basi, ni mfano jinsi gani! Je, maisha yetu yangeonyeshaje, kwa Yake? Naye alifanya mfano wa kile tunapaswa kufanya, jinsi tunavyopaswa kuwa. Tunapaswa kumwona wakati unatazama kwenye kioo. Mwone Kristo, kioo cha Neno Lake, jinsi alivyofanya hivyo kwa ajili ya upendo.

53 Na tukatoa mchezo mdogo wa kuigiza hivi majuzi usiku, wa Kristo kwenda juu Golgotha, na jinsi ambavyo nyayo, za Damu Yake ikitiririka mgongoni mwake, ambapo alikuwa amepigwa mijeledi, na kutendewa mabaya, na kuchubuliwa. Na haya yote, kwa ajili yako. Hakuwa na dhambi. Hakuwa na dhambi, lakini alifanywa dhambi kwa kufanyika sadaka ya dhambi.

54 Na sasa ilimbidi Mungu ku—kujidhihirisha katika sifa Zake, kwa Mtu huyu anayeitwa Kristo, ili kujitwalia kifo juu yake Mwenyewe. Kama Yehova, hangeweza kufa, kwa hivyo ilimbidi ajiumbie Mwenyewe mwili. Na hakuna mwanamke aliyeweza kuzaa mwili huo. Kwa hivyo tabia Yake Mwenyewe. . . Amina. Samahani. Nikifikiria hayo! Tabia yake ilionyesha Utu huo wenye upendo wa Yesu Kristo. Hakuna mwanamke aliyeweza kuileta. Mama ya Musa, yeye, Yokebedi, alikuwa mwanamke mashuhuri, na vile vile Rebeka na wanawake wengine wengi, lakini hakuna hata mmoja wao angeweza kuleta tabia ya aina hii, kwa sababu ilikuja kupitia kujuana kimwili na watu walioanguka. Lakini Mungu aliuleta mwili Wake Mwenyewe, makao Yake. Hiyo ndiyo sababu alikuwa Mwana wa Mungu, kwa sababu hakuna kitu kingine chochote kingaliweza kuionyesha. Lakini tabia Yake mwenyewe ya Kiungu ilidhihirisha maskani hii, ili kujidhihirisha Mwenyewe humo.

55 Na, hata hivyo, alijiondoa Mwenyewe kutoka kwa jambo kuu alilokuwa Yeye. Na wakati wa kuzaliwa Kwake, angeweza kuja na salamu kamili ya Malaika. Angeweza kuja na magari na Malaika wa Mbinguni, lakini Yeye alikuja kwa njia ya zizi. Hiyo ni ninii Wake—upendo Wake, akijishusha Mwenyewe chini kabisa.

56 Sasa, hebu iangalie tabia hiyo kidogo kisha ujiangalie, nami nijiangalie. Lakini, ndivyo alivyokuwa Yeye, ndivyo alivyokuwa Yeye, na ndiyo sababu alikuwa, kukuokoa. Alichukua. . . Yeye alifanyika wewe, ili uweze kuwa Yeye. Alichukua mzigo wako wa dhambi.

57 Kwa hivyo, tunapokuja kukutana na Yeye, hatutalazimika kusimama. . . Hatungeweza kusimama katika Uwepo wa Mungu. Hakuna njia ya sisi kuifanya. Lakini tunaposimama

ndani Yake, unaona, Yeye tayari ameitambua Dhabihu. “Huyu ni Mwanangu mpendwa Ambaye ninapendezwa Naye.” Aliitambua. Hakukuwa na kasoro yoyote Kwake. Na, hata hivyo, alipitia majaribu kama mtu mwingine yeyote. Hata hivyo, alidharauliwa. Alifanyiwa mzaha. Aliteswa, tangu saa ile alipozaliwa hadi saa ile alipokufa, na bado alirudisha mema kwa mabaya.

58 Huwezi, hakuna njia, kuwahi kupata Tabia kama hiyo; ila tu, kuikubali Tabia hiyo ndani yako. Kanisa haliwezi kufanya hivyo. Kanuni ya imani haiwezi kufanya hivyo. Dhehebu haliwezi kufanya hivyo. Elimu haiwezi kufanya hivyo. Lazima iwe ni Kuzaliwa. Lazima iwe ku—kufa, na kumruhusu Mungu aingie, kwa neema ya Kristo, aumbe tabia ya aina hii ndani yako, kusudi uwe Yeye, na maisha yako na Yake ni yale yale, basi nyinyi ni wana na binti za Mungu.

59 Basi, alipokuwa akipanda mlimani, na msalaba Wake ukiburuta na kufanya alama za miguu, loo, laiti ningekuwa msanii, laiti ningalikuwa, ningeongea ili niweze kukuchorea kiakili picha ya Kalvari, ya saa ile ya kutisha zaidi ambayo ulimwengu uliwahi kujua, na hata hivyo, hawakuwa na ufahamu wa kile kilichokuwa kikiendelea, mamilioni hawakujua.

60 Na je, ninaweza kugeuza picha hiyo kwa kile nilichosema wiki hii? Tunaingia tena saa ya kutisha, wakati wa kutisha. Na Phoenix na ulimwengu unatumbukia, na makanisa yanajitumbukiza yenyewe, katika ulimwengu, na katika maonyesho ya Hollywood, mmoja akimshinda mwingine. Na washiriki wetu wanakuwa wa kilimwengu. Inaonekana hawapati picha, na uzito, na ufunuo, wa kuonekana kwa Mwana wa Mungu katika siku hizi za mwisho.

61 Jinsi ulivyokuwa ni wakati mbaya! Walijua tu kwamba kulikuwa na mhalifu, chini ya adhabu ya kifo, alikuwa anaenda kufa asubuhi hiyo. Hiyo ndiyo yote iliyokuwa kwao.

62 Hayo ndiyo yote iliyo leo hii, kwa watu, wanaposikia Ujumbe. “Mtu mwingine mkorofi; mtakatifu mwingine anayejibingirisha; au shupavu wa kidini.” Na sisemi kwamba hakuna mashupavu wa kidini. Lakini hivi ulijua tu kwamba . . . Wanawaita, “Wa kipekee.” Vema, sikiza. Mtu yeyote anayeishi sawa ni wa kipekee, kwa ulimwengu huu wa kisasa. Sisi sote ni wa kipekee, tuseme. Na samahani tamshi hilo la kilimwengu, lakini ndiyo njia pekee niliyojua kwamba mngeweza kupata kile ninachokizungumza; unaona, mtu wa ajabu tu, wa kipekee.

Yesu alikuwa Mtu wa aina hiyo.

63 Manabii walikuwa watu wa aina hiyo, ambao walikuja katika enzi wakati kila kitu kilikuwa kikilegea. Nao manabii walikuja na kushika hizo sehemu legevu, wakazirudisha na kuzisukuma mbele za watu, na kuwaambia, “Mungu mwenyewe ambaye mnadai kumtumikia atawaangamiza, kwa sababu

mumeenda mbali na mpango Wake. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo Yeye anaweza kukuokoa." Na wao ni wa kipekee kila wakati.

64 Na, leo, tunaposikia Ujumbe wa Mungu ukitokea, tunafikiri ni upotovu, ushupavu, au kitu kingine. Na huko, kuna mengi ya hayo ulimwenguni: miradi, kutengeneza pesa, kutojali, watu chini ya mpagao na—na kunena kana kwamba ni Bwana. Bwana daima hujitambulisha Mwenyewe kwa njia ya kweli. Unaona? Basi angalia.

65 Lakini, katika hilo, je, ulijua kwamba vitu hivyo vyote havina budi kuja? Hakika. U—ua la waridi lazima liwe na miiba yake. Punje katika—katika karanga inapaswa kufunikwa na miibamiiba. Lazima uchimbe hiyo miiba ili uweze kufika kwenye kiini. Tunakosa tu kuona vitu hivyo. Vito, vyu—vyu—vyuma na vito, na pesa, fedha na dhahabu katika milima hii, zimefunikwa na uchafu, zimejaa dhahabu bandia na madini mengine ambayo huenda pamoja nayo. Tunatarajia hiyo. Huna budi kuichimbua uitoe. Wakati mtafuta madini anapata kile anachokiita "vumbi lenye madini," ni vumbi, lakini ni... Wanaiona. Inaashiria, huko ndani, kuna kivuli cha jiwe kubwa la madini mahali fulani.

66 Na wakati tukiwaona watu hawa leo wanaodhaniwa kuwa Wakristo, na wanaishi tu kwa njia yoyote ile, ni kitu gani? Ni vumbi lilipalo. Kuna jiwe kubwa la madini mahali fulani. Tunapoona mtu akijifanya kuwa na Roho Mtakatifu, wakati hawana, huku anaishi maisha tofauti, ni thibitisho tu kwamba kuna jiwe kubwa la Roho Mtakatifu halisi ambaye anaweza kumiminwa, anayeweza kutoa vitu ambavyo Yeye aliahidi. Lazima tuwe wenye kujali sana na wenye heshima.

67 Yesu, akienda juu. Ibilisi kila mara alitilia shaka kuwa Yeye ni zaidi ya nabii. Hakuamini kwamba Yeye alikuwa Imanueli. Mungu aliyedhihirishwa ndani ya Mwana Wake Mwenyewe, Yeye na Mwanawe wakiwa Mmoja, kwa nini, hangeweza kuona hilo. Je, Mungu, Muumba mkuu, angewezaje kusimama na kumruhusu mtu amwambie, "Vema, ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mkate"?

68 Na angewezaje Yeye, katika uga wa Pilato, wakati... Samahani tamshi hili; lakini wakati mambo yakiwa mabaya sana, kama tunavyoweza kuiita. Naye Huyo hapo amefungwa kitambaa usoni Mwake, na—na askari wa Kirumi wakimtemea mate usoni, na kung'oa ndevu, na Damu ikimwagika. Na taji ya miiba kichwani Mwake. Na tayari amepigwa, na Damu Yake ikitiririka kwa njia huru ubavuni Mwake. Na Shetani akiangalia hiyo. Na kisha kuweka kitambaa juu ya uso Wake, na askari wakampiga kichwani na fimbo, kisha wakapitishiana wao kwa wao, kasema, "Sasa, ikiwa unaweza kuona maono haya, ikiwa wewe ni nabii, sasa, wewe—wewe tuambie ni nani aliyekupiga."

Na kamwe hakufungua kinywa Chake. Kwa hivyo walifikiri kwamba . . .

69 Shetani alisema, “Huyo, huyo hawezi kuwa Mwana wa Mungu. Haiwezekani. Hangeweza kuvumilia hayo.” Lakini wana wa Mungu huvumilia chochote mradi tu wanajua wanafanya mapenzi ya Mungu. Na ndivyo alivyokuja kufanya. Ukosoaji!

70 Sasa, kwa Ujumbe wetu, tunaweza kusimama kwenye kioo cha kujitazama cha Neno la Mungu na kuona Kristo akijiakisi katika maisha yetu wenyewe basi? Je, tunaweza kuvumilia hayo, na aibu ya Ujumbe ambayo tunasimamia hapa? Mtu anaweza kusema kitu juu Yake, na hata hivyo bado hufungui kinywa chako wala husemi chochote juu yake. Alikuwa mfano, kwa sababu Mungu alikuwa akionyesha tabia Yake ndani Yake. Na kama sisi ni wana na binti za Mungu, Mungu huonyesha tabia Yake ndani yetu, basi tunakuwa kama Yeye. Hiyo ndiyo shauku ya moyo wangu. Nafikiri hiyo ni shauku ya kila mwaminio, ni kuwa kama Yeye zaidi.

71 Na kisha kwenye barabara juu ya kilima, wakati Shetani aliposema, “Sawa, kifo, sasa unajua nina amri yako. Na Yeye huyo yupo. Hatimaye tulimchosha. Imefikia mahali ambapo Yeye—Yeye yuko mwisho wa akili Zake. Hajui afanye nini tena. Amekuwa fedheha kati ya watu. Ujumbe Wake ukaanguka hewani. Na sasa serikali imemshika, naye ameshindwa. Yeye si Mungu. Nenda pale chini na udunge mwiba ndani Yake. Mwondoe maishani.”

72 Na njiani kwenda juu ya kilima, wakati nyuki alianza kupiga kelele kumzunguka. Lakini hiyo ndiyo sababu ilimbidi awe zaidi ya mwanadamu. Ikiwa angekuwa mwanadamu, au nabii tu, au kitu chochote pungufu ya Mungu, kama angekuwa hivyo, kifo kingemchoma na angelala kaburini.

73 Lakini nyuki wa mauti ni kama mdudu mwingine yeyote aliye na mwiba. Mwiba wake ukishikwa kwa kina, siku zake za kuuma zimeisha. Inavuta na kutoa mwiba wake.

74 Vema, maadamu mwili wa mwanadamu ulikuwa katika u—umbo la dhambi, aliyezaliwa kwa kujuana kimwili chini ya laana, basi kifo kilipouma nyama hiyo, mwiba ungeweza kurudi na kumchoma mwingine.

75 Lakini wakati alipouma nyama *hiyo*, ilichomoa mwiba wake nje. Hana mwiba tena. Alikuwa Mungu katika mwili, akikaa kati ya wanadamu. Siku zake za kuuma zilikuwa zimekwisha. Ndio maana ilibidi Mungu ajidhihirishe Mwenyewe katika mwili, ambao ni, tunajua kama Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Na alifanya hivyo ili aweze kuondoa adhabu.

76 Kwa sababu, unaona sasa, tunaenda kwenye sehemu nyingine ya Maandiko. Lakini unaona sasa kwa nini Mtu huyo alikuwa zaidi ya mwalimu tu, kama watu wanavyosema

ndivyo alivyo leo, mwanafalsafa, au Mtu mwema, au nabii. Alikuwa Imanueli. Alikuwa Mwana wa Mungu, ambaye ni Yehova Mungu aliyedhirishwa katika sifa Zake za kujidhihirisha Mwenyewe katika mwili aliojijengea, Mwenyewe. Amina. Ilijiakisi. Na asili ya dhambi ya mwanadamu haikuweza kufanya jambo alilolifanya. Unaona? Kwa hivyo ilibidi awe ni Mungu anayejitengeneza na kujidhihirisha Mwenyewe ndani ya Mtu, akifanya kioo, ili tuweze kumwona yule Mtu mkamilifu, ambaye ni Kristo. Ndiyo.

77 Hii, kwa kufanya hivyo, ilionyesha tabia Yake nzuri, yenye upendo. Unaona, ndani Yake kulikuwa na sifa kama Mwokozi, na ilibidi ijionyeshe yenyewe. Na Yeye hangeweza kuwa Mwokozi na kuwa mtu aliyezaliwa kimaumbile. Ilibidi awe zaidi ya mwanadamu. Naye alikuwa. Alikuwa Ndiye pekee aliyeweza kufanya hivi, kiasi kwamba kwa asili hakuwa na dhambi.

78 Alikuwa Mungu katika Neno. Sasa, Yohana Mtakatifu, sura ya kwanza, inaelezea jambo hilo. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili." Mungu alifanyika mwili wakati alijiwakilisha, au wakati alijidhihirisha Mwenyewe duniani, katika umbo la Mwanawe, Utu wa Yesu, Mwana wa Mungu. Mungu alijidhihirisha Mwenyewe katika Mtu huyo.

79 Je, Yesu hakusema, "Baba yangu na mimi ni Kitu kimoja. Baba yangu anakaa ndani Yangu. Sio Mimi nizifanyaye kazi hizo. Ni Baba Yangu. Yeye anakaa ndani Yangu. Sina mamlaka Yangu mwenyewe. Yeye hufanya hivyo." Chemchemi ya Mungu ya Neno, iliyoonyeshwa! Amina. Ninahisi upentekoste. Naam.

80 Kwa asili alikuwa hana dhambi, na hilo ndilo jambo pekee ambalo lingeweza kumdhihirisha huyo Mungu asiye na dhambi, Neno, Neno akiwa Mungu. Na neno ni wazo lililodhihirishwa. Na wakati Mungu alifikiria juu ya mzazi, alielezea wazo Lake, na—na Kristo alikuwa dhihirisho la Mungu. Amina. Unaiona? Alikuwa dhihirisho la Mungu, kwamba Mungu anaweza kuwa sisi na kuishi kama tunavyoishi, hata hivyo akidhihirisha kikamilifu kile mtu mkamilifu anapaswa kuwa, kikamilifu. Alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa na kuthibitishwa vizuri, kutambulishwa. Aliposimama hapa duniani, alisema, "Ikiwa sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi."

Tena akasema, "Ni yupi kati yenu anayeweza kunishtaki kwamba nina dhambi?"

81 Ningependa kuwafungulia hiyo kidogo tu, ikiwa inaruhusiwa. Mnaona, *dhambi* ni "kutokuamini." Kuna mambo mawili tu, njia, ambazo unaweza kuishi kwazo. Moja wapo ni imani, na ile nyingine ni kutokuamini. "Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari." Uvutaji sigara, kunywa pombe, uzinzi, kusema uwongo, wizi, kuiga mambo ya mwili, mambo hayo ni

sifa za kutokuamini. Ikiwa ungekuwa mwaminio, usingefanya mambo hayo. Hapana. Unafanya hivyo kwa sababu wewe si mwaminio.

Loo, wewe—wewe unasema, unasema, "Loo, lakini mimi ni mwaminio."

82 "Lakini kwa matunda yao mtawatambua." Unaona? Yako—matendo yako yanazungumza kwa sauti kubwa kuliko kile kukiri kwako kunathibitisha. Unaona? Usipoamini Neno la Mungu, na ukalihesabu kama kitu kilichopita, au kuchukua kitabu fulani badala Yake, na kusema, "*Hiki* ni kizuri tu kama Hilo," inaenda kuonyesha kuwa wewe si mwaminio. Hiyo ni kweli. Wewe—wewe siye. Na kama ungekuwa, basi ungeamini Neno la Mungu. Ingekuwa...Angejidhihirisha Mwenyewe kupitia Neno Lake.

83 Sasa, Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Basi Yeye akasema, "Sasa, ikiwa huwezi kuniamini Mimi," kasema, "amini kazi ninazofanya. Chunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Na hicho ndicho kitu chenyewe ambacho kinasema mimi ni Nani." Loo! Nashangaa ikiwa...?..."Tazama, Hicho Ndicho kinachosema kuwa mimi ni Nani. Maandiko yanasema kuwa Mimi ni Nani."

84 Basi acha nichukulie mbali kidogo, sivyo? Maandiko ndiyo yanayoelezea kile ulicho. Hiyo inakuelezea wewe na kunielezea mimi. Maandiko yanasema kile tulicho. Yana sauti kubwa sana hata sauti yetu haiwezi hata kusikika. Maisha yetu yanazungumza kwa sauti kubwa kuliko sauti yetu, ona, na ni njia ya Mungu ya kuturuhusu tuone kile tulicho.

85 Yesu alisema jambo lilo hilo. "Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yanathibitisha kile nilicho. Na ni yupi kati yenu anayeweza kunihukumu kwa kutokuamini, dhambi? Ikiwa sijafanya vizuri..." Sikiza, nazungumza juu ya kujiangalia mwenyewe. "Ikiwa sijajitambulisha Mwenyewe vizuri kuwa kile Neno lilisema kwamba nitakuwa!"

86 Ninashangaa kama sisi Wakristo tunaweza kuwazia jambo hilo usiku wa leo. Nashangaa ikiwa tunaweza kuangalia kwenye kioo cha Mungu cha kujitazama, ni mahitaji gani ya Mkristo, na kujitambulisha kwa njia hiyo. Nashangaa ikiwa tunaweza. Nashangaa kama tunaweza kujitambulisha usiku wa leo na Yohana 3:16, na, loo, aina nyingine zote za Maandiko; Marko sura ya 16, na sehemu hizi zingine zote, hapo, na huko katika—katika Wagalatia, naamini, na—na sehemu mbalimbali, Wathesalonike wa Pili, ambapo matunda ya Roho, na kadhalika. Nashangaa kama tunaweza kujitambua.

87 Yesu alisema, "Ni nani kati yenu anaweza kunishtaki, kwamba sijafanya na kufanya haswa yale Maandiko yalisema nitafanya." Hakuna mtu aliyeweza kusema neno, kwa sababu alikuwa amejitambulisha Mwenyewe kweli.

88 Nao, kama wanavyofanya siku zote, anayejifanya kuamini alikuwa amemtambulisha kama Beelzebuli, roho chafu. Alipojitambulisha Mwenyewe katika utambuzi wa roho, kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, basi walisema, "Hiyo ni roho chafu ndani Yake, inayofanya mambo haya." Kwa hivyo, unaona, alithibitishwa ipasavyo. Hakungeweza kuwa na kosa lolote.

89 Maskini yule mwanamke kisimani haku—hakufanya kosa lolote. Alisema, "Bwana, tunajua, wakati Masihi atakapokuja, atafanya mambo haya, lakini Wewe ni Nani?" Yeye . . .

Akasema, "Mimi Ndiye."

90 Na Mtu ambaye angeweza kufanya jambo kama hilo hakika angesema Ukweli. Kweli ya Mungu ilikuwa pamoja Naye. Nao waliagizwa, ikiwa nabii aliinuka na—na kumaliza, alisema kitu, na yale aliyosema yalitimia, alitambulishwa kama nabii. Naye alikuwa amemtambua Yeye kama nabii, na akauliza Yeye ni Nani. Naye akamwambia, basi hiyo ililitatua. Alikimbilia mjini na kusema, "Njoni, mwone Mtu Ambaye aliniambia mambo hayo." Hakukuwa na kosa juu yake.

Filipo hakuwa na kosa.

91 Ingawa, wakati, Nathanaeli, hasa, wakati Filipo alipokuwa amejaribu kumwambia kile kilichokuwa kimetokea wakati alipokutana na Simoni, lakini, Nathanaeli alipokuja, alikuwa na mashaka kidogo.

92 Lakini alipomwona Yesu, na Yesu akamwambia, "Tazama Mwisraeli, ambaye hana hila."

Akasema, "Rabi, ulinijua lini Wewe?"

93 Alisema, "Kabla Filipo hajakuita, nilikuona." Ha—hakukuwa na njia yoyote ya uwezekano wa kosa.

94 Akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

95 Yesu alisema, "Kwa sababu nimekuambia hivyo, unaamini. Unaweza kuona kubwa kuliko hiyo sasa."

96 Asili yake isiyo na dhambi ilidhihirisha Neno la Mungu. Unaona? Yeye alikuwa Neno, kwa hivyo Mungu alijidhihirisha Mwenyewe kwa asili hiyo isiyo na dhambi.

97 Naomba nisimame hapa sekunde moja tu. Sitaki kuwaweka muda mrefu sana, lakini inaonekana kuwa nzuri sana, kwangu mimi, kuzungumza na watu.

98 Angalia, ona, asili Yake isiyo na dhambi ilidhihirisha kile Yeye alichokuwa. Yeye, basi, ikiwa asili yake isiyo na dhambi, Mungu alijieleza kupitia asili hiyo isiyo na dhambi, inaonyesha kuwa asili yetu ni mbaya. Na haijalishi ni kiasi gani tunajaribu kuitia kiraka, au ni kiasi gani tunajaribu kuijumuisha na vitu vingine, haina budi kuwa haina dhambi kama ilivyokuwa Kwake, na kisha Neno la Mungu linaweza kuipitia.

99 Hiyo haimaanishi ukamilifu ndani yako binafsi. Huwezi kuwa hivyo. Lakini, unaona, hata watu wetu wanajiepusha na mazoea ya utakatifu. Tunaanza kulegeza kamba kwa wingi. Unaona? Hatuna budi kufikia mahali hapo pa maungamo yetu. Yeye ndiye kielelezo chetu, na Yeye ndiye Mbebaji wetu wa dhambi. Na kisha ikiwa tunakiri kwamba Yeye ni Mpatanishi wetu, Yeye ndiye Upatanisho wetu, basi ikiwa tunakiri hilo, basi hiyo inapaswa kumwakisi Yeye ndani yetu. Na sisi ni barua iliyoandikwa, kioo cha kutazama, ili watu waweze kumwona Kristo ndani yetu. Na sasa, ikiwa hawamwoni, basi sisi ni—tuna—tunaangalia kitu kingine, na hatumuangalii Yeye. "Mtazameni Yeye, miisho yote ya dunia, mpate kuishi." Njia pekee unayoweza. Ninii yake ya dhambi . . .

100 Asili isiyo na dhambi ilidhihirisha Neno la Mungu, sana, hata Yeye na Neno wakawa Mmoja. Alisema hivyo. "Mimi na Baba Yangu tu Mmoja. Mimi hufanya kila wakati kile kinachopendeza. Mimi na Baba yangu ni Mmoja tu." Alikuwa mkamilifu sana kwa mfano wa Mungu mpaka Yeye na Mungu walikuwa kitu kimoja kilichodhihirishwa. Alikuwa mwili, Mwana, aliyedhihirisha Uungu wa Mungu. Kwa hivyo hiyo ilimfanya Yeye kuwa uungu katika Mwanadamu, ili kumkomboa mwanadamu. Unaona? Yeye na Neno walikuwa Mmoja. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili." Kwa hivyo, Yeye na Neno wakawa kitu kimoja, ili Neno liweze kudhihirisha na liweze kuonyesha kwa ulimwengu Mfano wa kile mtu anapaswa kuwa.

101 Na mwanadamu hawezi kuwa hivyo ndani yake mwenyewe. Hakuna njia ya kuielimisha iingie ndani yake. Hakuna njia ya kujiunga nayo. Hakuna njia ya kuibatiza. Hakuna njia ya kufanya chochote kwake, ila tu kuiua.

102 Na acha izaliwe mara ya pili, na Asili mpya iingie. Hiyo ndiyo njia pekee, iue hiyo asili yako mwenyewe, ili uweze kuwa . . . Halafu Neno linakuwa kitu hai, linajidhihirisha tu Lenyewe kupitia wewe. Unaona? Halafu unatazama kwenye kioo cha kujitazama, wakati watu wanakuona kama kioo. Kwa sababu, unajua, Mungu amefanya njia. Watu hawatasoma Biblia, kwa hivyo Mungu amekufanya Biblia. Ndivyo ulivyo. Unachofanya, watu wanakuangalia.

103 Mungu alituma vioo Vyake, sura Yake—Yake—Yake Mwenyewe iliyodhihirishwa katika manabii, kwa sababu Neno lilikuja kwa manabii. Nao walimdhihirisha Mungu huko, hata hivyo, unabii wao ambao Mungu aliwapa.

104 Na sasa Mungu anajidhihirisha Mwenyewe kupitia Mwanawe, Kristo Yesu, anapotuchukua kama watoto waliopewa mamlaka, na kuweka Roho Wake ndani yetu, akilia, "Abba, Baba." Unaona? Au, kwa maneno mengine, "Mungu wangu, Mungu wangu!" Unaona? Kisha Roho Mtakatifu ndani

yetu, Roho wa Kristo akimdhihirisha Yesu Kristo, na watu wanakutazama. Unaona?

105 Na wanapoona unafiki na kila kitu, si ajabu, tumepoteza Nguvu zetu. Chumvi imepoteza ladha yake.

106 Loo, hakuna asili nyingine inayoweza kufanya hivi. Hapana. Maana, Yeye alikuwa ni tabia kamili ya Mungu.

107 Kwa maana, ilikuwa tabia iliyoanguka ambayo maumbile yote yalikuwa nayo. Wanadamu wote walikuwa na tabia iliyoanguka. Hata kila kitu ambacho kilikuwa chini ya mwanadamu kilianguka. Kila kitu kina tabia ya kufa.

108 Naye alikuwa na tabia iliyo hai, kwa hivyo aliidhihirisha ndani ya Kristo, Naye akalipa gharama hiyo. Na halafu kwa sababu ya utii Wake, alimfufua siku ya tatu. Unaona?

109 Na kisha Yeye hutupa sisi. Hiyo inatupatia sisi thi—thibitisho. Inatupa hakikisho, kwamba, mradi tuko ndani Yake, tayari tumefufuka pamoja na Yeye. Hatutafufuka pamoja na Kristo; tayari tumefufuka pamoja na Kristo. Hiyo ni kweli. Tuko ndani ya Kristo sasa. Na ikiwa Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, hivi hatujafufuliwa kutoka kwa wafu pamoja na Yeye? Amina. "Sasa tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni ndani Yake." Loo, jamani! Hiyo inapaswa kuwafanya ninyi Wapresbiteri kupaza sauti. Uh-huh. Naam. Hakika. Sura zinazoonekana za Mungu, zilizofinyangwa kwa mfano wa Kristo, ili ulimwengu uweze kumwona Yeye ndani yako. Hicho ndicho kioo cha kuangalilia.

110 Hakuna asili nyingine ingeweza kuifanya; ilikuwa imeanguka. Naye Mungu akatambulisha. Angalia. Mungu alijitambulisha Mwenyewe kama Mwanadamu, na kuchukua juu Yake mfano wa dhambi. Sasa, vema, sio dhambi, lakini mfano wa dhambi, ili apate kuchukua dhambi ya mwenye dhambi, unaona, na kulipa adhabu yake, na kumrudishia mwenye dhambi Uzima aliokuwa nao kabla ya kuanguka. Loo, jamani! Ni upendo ulioje Mungu aliotuonyesha! Unaona? Wazia hilo.

111 Na sasa kumbuka, baada ya Yesu kufanya hivi, wakati hakuna mtu mwingine aliyeweza kufanya hivyo, tunaalikwa. Sasa, kanisa, wazieni jambo hili kwa dakika moja. Tumealikwa kutengeneza tabia zetu kwa Zake, kwa neema Yake. Tumealikwa, wazia hilo, kuwa na tabia kama Yake. Ikiwa tuko tayari kuweka tabia yetu chini, na ufinyanzi tuliokuwa nao, "Wakaidi, wenye majivuno, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasingiziaji, na wasiotosheka, wanaodharau wale wanaojaribu kufanya mema, wenye mfano wa utauwa huku wakikana nguvu za Neno." Mungu anawezaje kuingia mahali kama hapo, wakati wao wanalikana Neno? Wakati, Yeye huangalia Neno Lake, kulithibitisha, kulifanya litimie. Nalo Neno linasukumwa nje, anawezaje kujitambulisha Mwenyewe na kitu kama hicho?

112 Hatuna budi kuchukua Injili yote, kamili. Inatubidi. Na sasa, kwa kuwa tumejitambulisha kama watu wa Injili yote, acha tuumbe tabia yetu. Tumealikwa kufinyangwa katika Sura Yake, ili tuweze kuonyesha Uwepo Wake. "Na kazi nizifanyazo mimi, nanyi pia mtazifanya. Maisha ninayoishi, nanyi pia mtayaishi." Tumealikwa, na Mungu, kumchukua kama Kielelezo, na kuacha tabia zetu zifanywe kama Yake. Jambo la jinsi gani! Jamani!

113 Halafu, tunaporuhusu tabia Yake iwe ndani yetu, basi tumekuwa wana, kwa kuwa na nia ya Kristo, nia, ambayo ndiyo tabia Yake. Nia yako huumba tabia yako. "Acha nia," Paulo alisema, "ya Kristo, nia hii iliyokuwa ndani ya Kristo, iwe ndani yako." Acha hiyo nia ya Kristo iwe ndani yako. Inaumba tabia ya mwana wa Mungu. Sasa, vipi . . .

114 Sikiliza tu kwa dakika moja. Tunawezaje kuwa na nia ya Kristo iliyokuwa ndani Yake, halafu tukane vitu ambavyo alituagiza tufanye? Tunawezaje kuweka miujiza katika wakati uliopita, wakati Kristo Mwenyewe alikuwa Mungu, na Mungu ndani yako. Uweponi mwa Mungu, daima kuna miujiza. Alisema, "Mnaniita Mimi 'Bwana.' Kwa nini mnaniita 'Bwana,' huku hamfanyi mambo ambayo nimewaamuru mfanye, niliyowawekea mfanye?" Hivi hamwoni ambapo tumefikia, ambapo kanisa linateleza? Na ninaipata sana kati ya Wapentekoste wetu, pia. Tunasonga mbali sana na hiyo Kambaokozi. Lazima turudi kwenye hiyo, rafiki, turudi, kwa sababu tunakuwa kubwa sasa.

115 Ninaona mahali ambapo chapisho la Wafanyabiashara ndilo kubwa zaidi, labda kama kile Oral Roberts alicho nacho. Nami nagundua kwamba tunapoanza kuwa wakubwa, basi tunaanza kutenda kama wakubwa, unaona, kama vile tu Israeli ilivyofanya. Na tunaanza kutenda kama tunajilinganisha tu na hao—hao wengine. Kumbuka, "Nyinyi ni watu tofauti. Nyinyi ni taifa takatifu, ukuhani wa kifalme, watu wa kipekee." Mbona, sisi Wapentekoste tulifikia ambapo sisi sio wa kipekee zaidi kuliko yeyote mwingine ulimwenguni. Tunavaa tu, tunatenda, tunazungumza, tunaenda na kufanya vitu wanavyofanya; kukimbia nyumbani, kuangalia televisheni, badala ya kukaa kwa ajili ya kanisa; na mambo yale yale tu wanayofanya, karibu. Tunajaribu kushindana, kujaribu kuwa kama akina Jones. Unaona? Hatutaki kufanya hivyo.

116 Tunataka kuwa, kuifanya Biblia hii kuwa kioo chetu cha kujitazama, na tujiruhusu tuumbike na tabia Yake; tukiwa na tabia Yake, nia Yake, tukiruhusu nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yetu. Nia yake daima ilikuwa . . .

117 Nia Yake ilikuwa ifanye nini, nia iliyokuwa ndani ya Kristo? Daima kudumu na Neno la Baba. Haijalishi ni nini kilionekana kung'aa, na ni nini kilionekana *hivi*, haikuleta tofauti yoyote Kwake. Neno la Baba ndilo lililojalisha. Kila

mahali, alipokutana na ibilisi, hakuwahi hata kutumia nguvu Zake kumshinda. Alitumia Neno, kwa sababu huyo alikuwa ni Yeye.

118 Hivi uliwahi kuwazia? Hakuwahi kuandika kitabu wakati alipokuwa duniani. Kadiri tujuavyo, Yeye hakuandika ila mara moja. Hiyo ilikuwa kwenye mchanga. Kisha akaifuta, labda, baadaye. Kwa nini hakuandika neno? Kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Unaona? Aliishi Neno. Hatuhitaji vitabu vingi sana, wakati unapokuwa barua ya Mungu iliyoandikwa. Unaona? Unaona? Hizo ndizo Mungu anataka muwe, sura Zake.

119 Unajua, katika ulimwengu wa makafiri, jinsi makafiri walivyojiwekea sanamu na wanasujudu mbele ya sanamu, na kujichochea kuingia katika mhemko mkubwa sana hata wanaamini wanaweza kusikia sanamu hiyo ikiwajibu. Ni jambo la akili, lakini jinsi lilivyo kinyume na Ukweli wa Mungu.

120 Mungu anakutaka wewe. Hataki sanamu. Wewe ndiye sura hai ya Mungu. Na wewe unasujudu mbele za Mungu, naye anakujaza na Yeye mwenyewe, nawe unamdhihirisha kama kioo cha kujitazama, Kanisa Lake.

121 Ni tofauti jinsi gani tuliyo nayo. Tunataka kuwa kama Presbiteri, Methodisti, na tuwe juu vile vile. Na kila kitu hakina budi kung'arishwa na kuwa cha hali ya juu. Na tunazidi kuwa mbaya. Unaona? Unaona? Tunayo. . . tunaondoka kwenye ule mstari ulioandaliwa. Rudini, kanisa. Ninawaonea shauku, kwa sababu Kuja kwa Bwana kumekaribia. Acha Yeye awe sura yako iliyodhihirishwa, akijidhihirisha Mwenyewe ndani yako, kwa sababu kila wakati Yeye alikuwa akifanya Neno la Mungu hasa.

122 Hivyo ndivyo manabii walivyofanya, kila mmoja. "Neno la Bwana liliwajia manabii." Na ndivyo walivyojua kuwa walikuwa. Musa, Neno la Bwana lilimjia Musa. Zaidi. . . Neno la Bwana lilimjia Nuhu. Neno la Bwana lilimjia Danieli. Neno la Bwana lilijidhihirisha Lenyewe kupitia watoto wa Kiebrania. Ilikuwa ni kitu gani? Wakati wanadamu, wa wakati wowote, walipochukua Neno la Mungu, ndipo Mungu aliwaelezea Neno hilo.

123 Nuhu alikuwa sura na ishara ya hukumu ya Mungu inayokuja, na alilidhihirisha Neno. Na kwa kudumu na Neno, Neno lile lile alilolidhihirisha, liliuhukumu ulimwengu na kuokoa nyumba yake mwenyewe.

124 Danieli alikuwa amekusudia moyoni mwake, hatajitia najisi na ulimwengu. Na ilifanya nini? Iliokoa maisha yake. Watoto wa Kiebrania, vivyo hivyo.

125 Na kila mtu aliyewahi kumtumikia Mungu, akawa mfano wa Mungu, alikuwa Mungu akidhihirisha Neno Lake mwenyewe kupitia wao. Kwa sababu, watoto wa Kiebrania walisema, "Mungu wetu anaweza kutukomboa." Hawakuwa na ufunuo juu yake, si zaidi ya hapo. "Lakini," kasema, "hata

hivyo, hatutaiinamia sanamu yako." Ilikuwa nini? Walikuwa wakionyesha imani yao katika Neno la Mungu. Naye Mungu akajidhihirisha Mwenyewe tena na kuakisi, naye alikuwa ndiye Mtu wa nne ambaye walimwona, kwenye kioo kile kule. Mungu, akijidhihirisha Mwenyewe kupitia sura Zake zilizo hai! Loo, jamani!

126 Sasa wacha tuangalie katika—katika kioo cha Mungu, Neno, na kutambua tabia yetu ya sasa. Sasa, naweza kuwachuna kidogo tu.

127 Sitachukua muda mwingi zaidi. Loo, jamani! Sikujua muda ulikuwa umeenda hivyo, imepita na robo. Sina saa hapa.

128 Niliangalia moja jana usiku, na kuhubiri kama masaa mawili. Nikawazia, "Jamani, ni saa moja tu. Ninaendelea vizuri, najipasha moto tu." Na hapa ilikuwa saa tatu na nusu, wakati wa kuondoka.

129 Angalia. Hatutakaa zaidi, hata hivyo. Ngoja niwape tu hii sasa hivi tu. Angalia. [Ndugu mmoja anasema, "Endelea kuhubiri."—Mh.] Angalia. Asante. Unajua, wakati . . .

130 Hebu tuone ikiwa tunaweza kujitambua wenyewe. Sasa sikiliza. Sikiza hili kwa makini, ninachosema sasa, tabia yetu ya sasa. Nitaenda polepole sana. Nataka iingie kwa kina kabisa sasa, kabla hatujafunga. Ikiwa ungaliishi katika siku za Nuhu . . . Sasa, wazia tu kuwa wewe ni nani. Kuwa mkweli kwako mwenyewe. Sababu, ikiwa hutakuwa mkweli kwako mwenyewe, huwezi kuwa mkweli kwa Mungu.

131 Kama ungeishi katika siku za Nuhu, na ulikuwa katika tabia yako ya sasa, ungetambuliwa na kikundi gani? Sasa wazia hilo. Kundi gani?

132 Wakati, huyu hapa mzee mlokole amesimama pale juu kwenye kilima, ambaye imethibitika, tena na tena, kwa miaka mia na ishirini, kwamba amerukwa na akili, kwa sababu anabashiri haswa kwamba kuna maji yanayoshuka kutoka huko juu. Na vyombo vyao vyote vya kisayansi vinathibitisha kuwa hayakuwepo. Na kwa sababu haikukubaliana na vitu vyao vya kisayansi, Mungu Mwenyezi angewezaje kufanya kitu ambacho kilikuwa kinyume na mawazo yao? Unaona? Na mtu huyo alizungumziwa. Alikuwa ndiye kichekesho cha wakati huo.

133 Sasa, najiuliza. Naam. Uliza tu kwamba, ungetambulishwa na kikundi gani? Na maoni maarufu ya siku hiyo?

134 Loo, unasema, "Mimi—mimi ni wa kanisa." Hiyo siyo ninayozungumzia. Walikuwa na vikundi vingi vya kanisa katika siku hiyo, labda zaidi ya waliyo nayo sasa.

135 Lakini kulikuwa na mtu aliye na u—ujumbe kutoka kwa Mungu. Hiyo ni kweli. Na haikupendwa sana na watu. Kundi lake lilikuwa lisilopendwa sana, maana alidhaniwa kuwa

mlokole. Je, ungekuwa tayari kujitambulisha na kikundi hicho cha washupavu?

136 Njia pekee ambayo ungeweza kuifanya, ingekuwa kwamba ifunuliwe kwako binafsi. Na hivi ulijua kwamba hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu alijenga Kanisa Lake?

137 Angalia katika bustani ya Edeni, je, Habili alijuaje kuwa ni damu badala ya tofaa? Loo! Unaona? Ilifunuliwa kiroho.

138 Na, angalia, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, alisema, wakati huo mashuhuri aliokuwa akisema, "Watu wanasema mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?"

"Baadhi yao walisema, mbona, Wewe ni 'Musa,' au Wewe ni 'Yeremia,' au 'mmoja wa manabii.'"

139 Akasema, "Lakini mimi ni—ninakuja moja kwa moja kwenye hoja. Unafikiri nini kuhusu Hilo? Unaona? Si kile mtu mwingine anasema sasa, bali nataka kujua wewe unafikiria nini juu Yake?"

140 Na hapo ndipo Petro alipozungumza na kusema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

Sasa angalia jinsi alivyonukuu hilo.

141 Sasa, tunajua kwamba kanisa Katoliki, sio kuumiza hisia zenu Wakatoliki, lakini mlisema Yeye alilijenga juu ya Petro, akiwa ni jiwe dogo. "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu. Malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Unaona? Sasa, ikiwa ndivyo ilivyo, basi kanisa limerudi nyuma. Unaona? Sasa, basi, ikiwa ndivyo ilivyokuwa, lilijengwa juu ya mtu.

142 Sasa, Mprotestanti anasema alilijenga juu Yake mwenyewe, ambaye alikuwa Jiwe kuu la Pembeni, Mwamba. Na, hiyo, hiyo ina Ukweli mwingi kwake.

143 Lakini hebu niingize tu kitu kingine katika hiyo, ku—kukaza tu kidogo. Sitakubaliana na wote wawili, kwa kusema hivi, kwamba hakuwa anazungumza juu Yake Mwenyewe, moja kwa moja, lakini kwa uwezekano alikuwa anazungumza juu Yake Mwenyewe. Wala hakumjumuisha Petro zaidi ya kukiri kwake hivyo.

144 Kwa sababu, angalia kile Yeye alichosema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwani mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza hili kwa uzoefu fulani wa seminari, au mtu fulani alikuambia juu yake. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili."

145 Basi, ni ufunuo wa kiroho wa kuwa Yesu Kristo ni Nani. Ni hakika. Ndipo akasema, "Juu ya mwamba huu, juu ya ufunuo wa kiroho, nitalijenga Kanisa Langu." Ilionyesha malango yote ya kuzimu yatakuwa dhidi yake, lakini hayatalishinda. Unaona? "Nitajenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayataweza kushinda Kanisa hili."

146 Kwa hivyo, unaona, Nuhu alikuwa na ufunuo wa kiroho. Mungu alikuwa amezungumza naye moja kwa moja. Habili . . .

147 Wakati Kaini alitoa matunda ya kondeni, kama matofaa na matunda, na kadhalika, na akaipamba madhabahu yake, na kusema, "Mungu atakubali hii kwa sababu nimefanya *haya* yote, na kuandaa madhabahu kubwa. Na nimepamba. Niliifanya kuwa ya kupendeza. Tunalo kanisa kubwa zaidi jijini, au kadhalika. Mungu atalikubali, katika hili." Yeye hakubali kazi ya mikono ya mtu yeyote, katika ukombozi.

148 Lakini Habili alileta mwana-kondoo na kutoa damu, na Mungu alishuhudia kwamba alikuwa mwenye haki. Aliijuaje? Hakukuwa na Neno lililoandikwa siku hizo. Ilikuwa ni ufunuo, na ndivyo ilivyo leo.

149 Unasema, "Vema, mimi ni wa kanisa. Kanisa langu ni zuri tu kama kanisa lako. Yote yametengenezwa na aina moja ya jengo, vifaa vya aina moja." Hiyo ni kweli. Jengo halihusiani nalo.

150 Shirika ni kikundi cha wanadamu wanaokusanyika pamoja, wanafanya uamuzi wa kile wanachosimamia, na ndivyo ilivyo. Sina chochote dhidi ya hiyo, hiyo ni sawa, lakini hiyo siyo ninayozungumzia. Unavaa nguo za aina ile ile, labda, zikiwa ni nzuri, kile waaminio wengine wangefanya, na bado hiyo haifai kitu.

151 Lakini sasa angalia hapa. Kile kilicho, ni ufunuo wa kiroho wa Neno la Mungu. Kwamba, kila kitu kingine ni kibaya isipokuwa Neno hilo, nawe unaliamini. Yeye alikuwa Neno, na Yeye ndiye Neno, na Yeye atakuwa Neno daima. Na wakati Mungu anaweza kufungua mkondo huo, basi anaweza kutiririka kwa njia huru kupitia ule mwili uliotakaswa. Sasa, sasa, sasa tunaona jambo hilo.

152 Ikiwa ungekuwa katika siku hiyo, ungetambulishwa na kikundi gani; pamoja na nabii, pamoja na Neno lililothibitishwa, ingawa walikuwa katika uchache? Au, ungekuwa na watu wenye maoni yanayopendwa na watu? "Vema, nakwambia, naamini mtu huyo ni mwendawazimu." Na njia pekee ambayo ungeweza kujua hakuwa mwendawazimu ni kwa Mungu huyo huyo kukufunulia kitu kile kile alichokuwa amemfunulia Musa.

153 Na njia pekee ambayo tutaweza kuwa sura za Mungu, na wana wa Mungu, ni kwa Mungu kutufunulia, na kujidhihirisha Mwenyewe kupitia Neno Lake, kwetu, na sisi kwa ulimwengu. Huo ndio mkondo pekee. Kwa kuwa, Kristo alikuwa ndiye Sura hapa duniani, ambayo ungeweza kuona, Mungu katika Mtu, alionyesha Sura ya Mungu, kwa sababu Mungu alikuwa ndani Yake sana hata walikuwa Mmoja. Na sasa wakati Kristo alipoondoka, alilitakasa Kanisa, ili Kanisa lichukue nafasi Yake na kudhihirisha Neno la Mungu. Mnaona? Hiyo ndiyo njia pekee inayoweza kufanywa. Loo, jamani!

154 Je, ungekuwa na watu maarufu ambao walikuwa na maoni yanayopendwa na watu? "Maadamu mimi ni mfuasi wa kanisa!" Na labda, "Kwa sababu nilicheza katika Roho, niko sawa." Labda, "Kwa sababu nimenena kwa lugha, niko sawa." Au labda, "Tunaye mchungaji mzuri, na mimi niko sawa." Sasa, vitu hivyo ni vya uaminifu. Sina la kusema dhidi ya hilo. Hiyo ni kweli.

155 Lakini mpango huu wa wokovu ni jambo la kibinafsi kwako. Kunena kwa lugha ni karama ya Mungu. Kucheza katika Roho ni Uwepo na Utukufu wa Mungu. Lakini kwako kuruhusu tabia yako iumbike katika sura ya Mungu, kwamba Yeye hujionyesha Mwenyewe, na wewe ni—na wewe ni sanamu Yake, inayotembea juu ya nchi, sura Yake iliyodhihirishwa.

156 Sasa, je, ungekuwa tayari kufanya hivyo katika siku za Nuhu? Au ungekuwa upande wa ukosoaji, ukikosoa nabii na ujumbe wake uliotumwa na Mungu? Sasa wazia hilo. Ni upande gani ungefikiria, katika hali yako ya sasa, ungechukua? Sasa kuwa mkweli. [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] (Samahani.) Hakuna haja ya mimi kujaribu kusema hilo. Wewe, huna budi kuliwazia, wewe mwenyewe.

157 Au katika siku za Eliya, wakati aliongea vya kutosha juu ya nyuso zilizopakwa rangi, na—na yule mama wa kisasa wa majira haya, yule Yezebeli, ameketi pale akigeuza ki—kichwa cha mumewe kwa njia yoyote kilichotaka kwenda? Na iwe kilitaka au la, alikigeuza, hata hivyo. Na wahubiri wote wakikubali, "Hiyo ni sawa. Tazama, hiyo ni sawa, kwa sababu malkia wetu!" Unaona? Na wote ni rahisi kuanguka katika mkondo huo.

158 Ikiwa hiyo si picha ya leo, sijawahi kuiona. Mambo haya yote ya kijinga ambayo watu wanafanya, na, hata hivyo, katika Jina la Kristo. Ikiwa alikuwa na hatia ya yote hayo? Yeye hana hatia ya yoyote yake. Unajuaje mahali Yeye . . .

Neno linalielezea. Hebu tufuatilie tu dakika chache tuone.

159 Je, ungekuwa upande wa kukosoa? Je, ungekuwa pale chini na Eliya, ukisimama pale wakati Eliya alionekana kuwa ndiye wa pekee peke yake, na kila mtu alidhani alikuwa mzee aliyechanganyikiwa au kitu fulani? Lakini hiyo haikumsumbua hata kidogo. Alikuwa na Neno. Naye alikuwa na Neno, na hakuogopa na Neno. Hakuwa na hofu, Nalo. Mtu yeyote aliye na Ujumbe wa Mungu haogopi chochote. Hiyo ni kweli.

160 Maskini Stefano wa kale alisimama asubuhi hiyo mbele ya Sanhedrin, alisema, "Kwa nini, enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyoni na masikioni, mnampinga Roho Mtakatifu kila wakati. Kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo."

161 Biblia ilisema, "Uso wake ulikuwa kama Malaika." Siamini, ni kama taa ya umeme au kitu fulani. Malaika anajua mahali anaposimama. Malaika haogopi chochote. Yeye ni Mjumbe kutoka kwa Mungu.

162 Na mtu yeyote aliye na Ujumbe wa Mungu anajua ni wapi anaposimama. Hajali mtu yeyote, kile walicho nacho kusema juu Yake. Hakuna maaskofu wala kitu kingine chochote kinachomsukuma. Anajua mahali hasa anaposimama, na hiyo inatosha. Mungu huthibitisha Ujumbe wake na kuthibitisha ya kwamba ni kweli, kwa hivyo anasimama moja kwa moja na Huo. Haogopi. Hiyo ndiyo sura ya Mungu iliyodhihirishwa.

163 Ndivyo Yesu alivyofanya. Hakuogopa kusema, "Loo, enyi Mafarisayo vipofu, nyinyi—nyinyi ndio mnaojenga makaburi ya manabii, na nyinyi ndio mliowaweka humo. Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi," na maaskofu wakuu na kila kitu kingine. Hakuogopa, kwa sababu alijua mahali alipokuwa. Naam.

Katika siku za Eliya, ungechukua upande gani?

164 Au, katika siku za Musa, wakati kulikuwa na ujumbe wa Mungu, uliothibitishwa kabisa. Sasa sikiliza. Katika tabia yako ya sasa, unasema, "Mimi ni Mkristo." Sawa. Nitakuuliza tu, tabia yako ya sasa, ungechukua msimamo gani? Wakati, Dathani alipoinuka na kusema, "Sasa ngoja kidogo. Kuna wanaume wengi watakatifu hapa kando na wewe, Musa. Tutachukua tu kikundi cha wanaume na kujifanyia jambo kubwa hapa. Na jambo la kwanza unajua, tutakuwa na maaskofu na maaskofu wakuu, na kila kitu kingine, karibu hapa. Na Mungu yuko ndani ya watu Wake, kitu chote. Usifikirie kuwa wewe ndiye changarawe pekee ufukoni." Wakati, Dathani aliposimama pale, akasema, "Je, ninyi watu hamfikirii hivyo? Mtu huyo hujichukulia mengi sana mikononi mwake. Anajaribu, kutuambia cha kufanya. Kwa nini, katika wingi wa—wa wengi kuna ushauri, kuna—kuna usalama. Kwa nini, sisi sote tunapaswa kuja pamoja na kutatua jambo hili." Lakini kulikuwa na ujumbe wa Mungu, ulithibitisha ujumbe wake.

165 Hatupaswi kumwuliza mtu mwingine kitu kuhusu Ujumbe huu ambao tunahubiri. Umeandikwa hapa katika Biblia, na Mungu anathibitisha kuwa ni kweli. Basi ni kwa nini inakubidi kutoka na kusema, "Sasa, wewe Mkatoliki, tufanye nini kuhusu *hili*? Tutajiunga na Shi—Shirikisho la Makanisa. Tutajua. Tutaungana pamoja na hao ndugu na kuona jinsi walivyojenga vikundi vyao mashuhuri." Sisi watu wa kipentekoste hatuhitaji hiyo. Hatuna haja ya kujiunga na Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Tunahitaji kujiunga na bendi ya Mbinguni, nguvu ya kipentekoste, kuinuliwa juu kwenda mahali pa Mbinguni. Hatuhitaji vitu hivyo.

166 Lakini, unaona, ungechukua upande gani, katika tabia yako ya sasa, ikiwa Dathani angeinuka na kusema hivyo, na wewe ungekuwa umesimama pale wakati huo? Je, ungeshikilia ujumbe na mjumbe wa Mungu, na kukaa nao, na kuthibitishwa kabisa kuwa ni Kweli? Au, ungechukua ma—makaratasi yako

na kwenda huko na kujiunga na kikundi kingine? Loo, hiyo, unaona, wazia tu juu yake.

167 Wakati ilionekana kuwa yote yalikuwa dhidi ya ujumbe wa Mungu uliothibitishwa na mjumbe wa wakati huo, mambo yalikuwa mabaya sana kwa Musa. Kila kitu kilikuwa kimeenda, ilionekana kana kwamba Mungu alikuwa amemwacha. Lakini walikuwa wamemwona Mungu akifanya jambo. Walijua Mungu alikuwa ndani yake.

168 Sasa, au, katika siku za Kristo...Tutaharakisha. Katika siku za Kristo, ungechukua upande gani, wakati makanisa yote makubwa na wanatheolojia wao wa kisasa na walimu walipokuwa wakimpinga Yeye na kanuni Zake, na Mafundisho wazi ya Maandiko? Waliyapinga Hayo. Wakati kanisa lako ulilokwenda lilisema, "Jamaa huyo ni mlokole. Vema, hakutoka kwenye seminari zetu. Hatuna rekodi ya yeye kwenda shule zetu. Hana kadi ya ushirika. Hana hati zozote za utambulisho. Kwa hivyo, huyo mtu ni mwendawazimu. Usiwe na uhusiano wowote na Hiyo," ungefanya nini katika hali yako ya sasa? Uliza tu kwa dakika moja. Sawa. Je, ungefanya nini? Ikiwa Yeye...

169 Ikiwa ungeishi katika siku hiyo, na ulikuwa wa sa—sa—Sanhedrin, na hiyo ni kama ba—Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na kanisa lako lilikuwa limeungana na hilo, na wangekuwa wamechukua vitu hivi vyote. Na Mtu huyu aliinuka, nawe ukamwona akifanya kazi za Mungu, na hakuna mtu aliyeweza kushindana Naye. Hata hivyo, alidhaniwa kuwa "Mtu kichaa, aliyerukwa na akili Zake." Alikuwa...

170 Mungu anisamehe kwa tamshi hili, lakini Yeye alikuwa mmoja wa "wa kipekee" wa siku hiyo. Tazama, ninataja hiyo ili uweze kuelewa.

171 Kwa nini? Alizaliwa Mbinguni. Tabia yake ilikuwa Juu. Haikuninii—haikuenda sawa na ushirika wa mashirikisho ya ulimwengu huu. Unaona? Hakuwa mtu wa aina hiyo. Ingesimama wapi wakati mwanatheolojia wote, walimu wote, wanasema, "Je, Mtu huyu alitoka wapi? Hatujui hata mahali alikotoka"?

172 Alipomponya yule kipofu, walisema, "Mbona, hatujui Mtu huyu ametoka wapi. Mpe Mungu utukufu. Hatujui chochote kuhusu Mtu huyu. Alitoka wapi? Sisi, hatuna kumbukumbu Zake. Yeye hayuko kwenye ratiba yetu. Yeye hayuko kwenye halmashauri yetu ya wakurugenzi. Yeye, Yeye hayupo popote. Hakuna hata mmoja wao ajuaye chochote kumhusu. Alitoka wapi?"

173 Yule kipofu akasema, "Hilo ni jambo la kushangaza, kwamba Mtu anaweza kufungua macho yangu, na hata hivyo nyinyi hamjui ametoka wapi. Nanyi mnadhaniwa kuwa ndio viongozi wa siku hii." Naam. Kasema, "Sasa, ikiwa Yeye ni mwenye dhambi au la, siwezi kusema hilo. Mimi si

mwanatheolojia. Lakini jambo moja najua: ambapo nilikuwa kipofu, sasa ninaweza kuona." Hayo tu. Hayo ndiyo muhimu. Alitaka kuona. Naam.

174 Kwa kweli, wote wa kisasa, walimu wote wa Biblia walikuwa wakimpinga Yeye na Neno Lake la kweli kutoka kwa Mungu. Unaamini alikuwa wa kimsingi kabisa, sivyo, katika mafundisho Yake? Lakini sio kulingana na shule zao. Je, hiyo ilizama ndani? Tulijuaje kwamba Yeye alikuwa wa kimsingi? Akawauliza, "Ni nani anayeweza kunithibitisha kuwa nina dhambi? Tafuta Maandiko. Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yanakwambia haswa. Sasa, ikiwa sifanyi kile Maandiko yanasema, basi Baba hathibitishi hilo kupitia Mimi, basi nitupeni nje; nimekosea." Naam, bwana. Sasa, tunaona ya kwamba walikuwa wanapinga Hilo, Neno la kweli la Mungu.

175 Loo, hali yako ya sasa ingekutambulisha na Yeye, au na kundi lile la Mafarisayo waliopofushwa? Je, hali yako ya sasa, ungeshikilia ka—kanuni zako za imani ya kanisa lako? Je, ungeishikilia kwa sababu mchungaji wako alikuwa, labda, ungesema, "Naam, yeye ni mtu mzuri"? Anaweza kuwa mtu mzuri na bado awe kipofu. Hakika. Hivi Yesu hakusema, "Enyi viongozi vipofu wa vipofu"?

176 Sasa, katika hali yako, fikiria tu sasa, ungefanya nini? Unatambuliwa wapi kati ya umati wa watu huko? Hali yako ya sasa ni nini? Je, ungekuwa pamoja na yule Farisayo, "Vema, nakwambia, mama yangu alikuwa mfuasi wa kanisa *hili*, na hiyo ni nzuri tu kama yeyote kati yao. Nitabaki papa hapa tu"? Unaona?

177 Na ulipoliona Neno la Mungu limethibitishwa, Hilo ni Kweli, na mjumbe, nawe ukayachunguza Maandiko na kuyajua. Lakini dhe—dhehebu lako lilisema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho." Sasa, ungefanya nini katika hali yako ya sasa? Wengi wenu mmelielezea.

178 Ikiwa ungesema moyoni mwako sasa, "Hapana, nisingekuwa pamoja na hao Mafarisayo. Nisingetambulishwa pamoja nao," basi vipi sasa? Maandiko yanasema Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Na sasa je? Unasema, "Nisingetambulishwa na Mafarisayo." Na sasa je? Unajua, historia inajirudia. Nilikata kipande kutoka kwenye gazeti, hivi majuzi, juu ya hilo. Mafarisayo wa siku hiyo walichukua msimamo dhidi Yake, kwa sababu ya chuki. Ndivyo wanavyofanya leo.

179 Kumbuka, Nikodemo alisema jambo lile lile. Alisema, "Rabi, tunajua kwamba Wewe ni mwalimu uliyekuja kutoka kwa Mungu."

180 Lakini kwa sababu kwamba kanuni zao za imani na madhehebu hayangekubali ujumbe Wake, basi wakamkataza mtu mwingine yeyote. Alisema, "Hutaingia, wewe mwenyewe,

na unawakataza wengine wasiingie." Ndiyo. Hali iliyoje! Sijui kama tungeweza kujitambulisha na kitu kama hicho?

181 Ikiwa ungemfuata ili tu uone miujiza Yake, kama wengi walivyofanya, na ulimfuata leo kanisani, ili tu uone miujiza Yake na kukaa karibu. Lakini kuweka mkono wako chini, kupokea Roho Mtakatifu, wewe mwenyewe, hutafanya hivyo. Hawatafanya hivyo. Wengi walimfuata kwa ajili ya miujiza Yake tu, kuiona. Lakini alipokaa kwenye Mafundisho halisi ya Maandiko, umati ulimwacha.

182 Wakati, wangemwona akiponya wagonjwa na kufungua macho. Na mtu angeweza kugusa vazi Lake, Naye angegeuka, awaambie mambo hayo. Na kumwambia Filipo na Nathanaeli, na hawa wote, mambo hayo. Mbona, mwanamke kisimani, na vitu hivi vyote, kwamba alijitambulisha Mwenyewe kuwa ndiye na—nabii ambaye Musa alinena juu yake, Kristo, Masihi. Wakati hawakuwa na nabii kwa miaka mia nne, halafu jukwaani akatokea huyu Yesu, akithibitisha Yeye alikuwa ndiye, unaona, kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

183 Wengi wao walikuwa wamemfuata kwa sababu, sehemu ya kwanza ya huduma Yake, alikwenda kutoka kanisa hadi kanisa. Loo, walimpokea kwa furaha, na wakampa mkono mkubwa. "Loo, Rabi, loo, Wewe ni mtu mashuhuri!" Lakini siku moja Yeye aliketi chini na Ukweli wa Kimaandiko. Na ndipo alipojitambulisha Mwenyewe, sio tu kama Mponyaji, bali kama *aliyetumwa-kutoka kwa-Mungu*, aliye na Ukweli na Uzima, wakati alipojitambulisha Mwenyewe kwa Hilo, loo, Hiyo ilikuwa kinyume na mapokeo yao, hata kwa wengi waliomfuata.

184 Hao sabini wakageuka na kuenda zao. Wewe ungefanya nini? Sasa, wazia jambo hilo. Wakati, Mtu ambaye ulikuwa umemwona akifanya ishara zile zile za Masihi, na kujua kwamba Masihi alikuwa anakuja, Naye alikuwa ametabiri haya yote kutokea, hata kwa Yohana na wao, na Yeye alikuwa ameyazungumza, kabisa, halafu ukamfuata na ukaona ishara kubwa ya Masihi, ikithibitisha kwamba hakuna hata mmoja wa wachungaji ambaye angeweza kustahimili Ujumbe huo, hata kidogo, halafu basi, mara moja, Yeye anakuja na kufundisha kitu ambacho ni Neno la Mungu haswa, lakini kinyume na njia yako ambayo umefundishwa, basi, ungeshikilia na mila yako? Je, ungeenda na wale sabini? Loo, Maandiko, Neno wazi kabisa! Je, ungeenda na wale sabini?

185 Au—au, unaweza kuona sasa utambulisho wako, mahali ungesimama? Sasa fikiria kwa kina, kwa unyofu. Ungesimama wapi sasa, na hali yako ya sasa? Wapi, ungetambuliwa katika kikundi gani, huko? Au, ungeweza kujitambulisha? Kwa haraka tu sasa. Je, ungeweza kujitambulisha na hiyo?

186 Nitazungumza na watoto hapa, matineja. Je, ungeweza kujitambulisha leo, ewe kijana, kama mwaminio anayekiri,

kama yule mtawala kijana tajiri, aina ya Elvis Presley anayependa raha za ulimwengu kuliko unavyopenda kumfuata Kristo? Je, utajitambulisha na kikundi hiki cha siku hizi, na, useme, sawa, kama huyu Bw. Presley? Kama ninavyoelewa, yeye ni Mpentekoste. Na Mpentekoste, kwenda na kutenda namna hiyo, yeye ni Mpentekoste tu kwa jina. Kwangu mimi, ni Yuda mwingine.

187 Pat Boone na wale watu wanaodai kuwa wa kidini, na hizo roki na kunengua, na uchafu wa ulimwengu, halafu wanadai Ukristo. Kwa nini, ni aibu. Ni mbaya zaidi kuliko mwuza pombe haramu. Ni mbaya zaidi kuliko—kuliko kahaba barabarani. Mungu angemheshimu kahaba kuliko hiyo.

188 Ernie Ford na wao husimama usiku kucha, hizi sherehe za vifijo na kila kitu, na kufanya yasiyofaa, huku mikono ikiwa imewakumbatia wanawake, hao wanaovutia kingono na kadhalika, halafu watoke na kuimba nyimbo. Hapo ni wakati umeuza haki yako ya kuzaliwa. Unawezaje kujitambulisha?

189 Kijana huyo mchanga alikuwa na . . . Alikuwa mtu tajiri. Alikuwa na nafasi. Yeye, labda amekuwa, mfanyabiashara Mkristo, pia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kanisa.

190 Sasa, kijana, ungefanya nini kuhusu hilo? Wakati, unajaribu kutenda kama Marilyn Monroe au baadhi ya hao wengine, au baadhi ya wanawake wengine kama mama taifa wa nchi, na haya hapa kila aina ya kufanya yasiyofaa, na huku kukata nywele, na—na kupaka rangi kwenye uso, na hizi nguo za kubana, za kizinifu. Na—na ninyi wanaume, mnawaacha wafanye hayo!

191 Na ninyi wachungaji, hamna ujasiri wa kuikemea kutoka kwenye mimbara, pia! Kweli. Kweli. Hiyo ni kweli. Naam. Hiyo ni kweli. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Sasa, hebu kidogo. Sikiza. Hiyo ni kweli.

192 Lakini mara nyingi mna wachungaji waliotumwa na Mungu ambao wataikemea, na bado hutajiambatanisha na Neno. Sasa sikiliza, tunapata, chukua, nenda kwa njia nyingine, pia. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Hiyo ni kweli. Ninaweka nini mbele zenu? "Loo," sema, "wao . . . " Najua bora kuliko hivyo. Nimepitia, mwenyewe, Phoenix, kwa miaka kumi na mitano iliyopita, na bado inaonekana sawa na ilivyokuwa siku zote, ikizidi tu kuwa mbaya. Kwa hivyo usiweke yote juu ya mchungaji. Uh-huh. Hebu tuseme tu sisi sote tuna hatia, na kusimama pale na tujiangalie kwenye kioo. Naam.

193 Kijana, vipi kuhusu hilo? Unapenda sifa za watu hao kuliko unavyopenda mwa—mwaliko unaopewa, kufinyanga tabia yako kuwa mfano wa Mwana wa Mungu? Vipi kuhusu hilo? Tunawezaje kufanya hilo? Loo, jamani! Je, unaweza kujiona unatambulika, unapenda-umaarufu? Vipi kuhusu . . .

194 Sasa, ninashuka kuja nyumbani karibu kidogo tu sasa. Vipi kuhusu ninyi Wapentekoste mnaojua vizuri zaidi? Hiyo ni sawa. Unajua bora kuliko hiyo. Unajua vizuri zaidi.

195 Kwa hivyo, kumbuka utambulisho wa mwisho wa mtawala huyu kijana tajiri. Alikuwa kuzimuni, akiangalia juu kwa mtu aliyekuwa ameishi sawa, akiomba maji. Lakini alikuwa amevuka pengo lile kubwa bila kukubali uwezo wa Mungu wa kumrudisha. Naye huyo hapo, naye angali huko hata usiku wa leo, na atakuwako siku zote. Sawa. Huo ndio utambulisho wake wa mwisho.

196 Kwa hivyo, usijitambulishe na malkia fulani maarufu wa ngono. Au, usijitambulishe na mmoja wa hawa hapa kina Elvis Presley wenye vichwa bapa, ukiendelea hapa na roki zako na kujinengua, na kujiita Mkristo; au Pat Boone fulani, kwa sababu una gita na unaweza kusimama nje na kutenda kwa ujinga nayo.

Hebu Kristo ajiakisi Mwenyewe ndani yako. Hiyo ni sawa.

197 Wapentekoste, leo, wanajitenga na Neno la Mungu.

198 Je, unajitambulisha na kikundi cha Yuda? Kumbuka, Yuda alianza, kutembea pamoja Naye. Sasa, ikiwa hii inaumiza, siikusudii kuumiza, lakini namaanisha kwa kufinya sana. Unaona? Naam. Yuda alianza vizuri. Alianza mwendo, kutembea pamoja Naye. Lakini alipofikia kuwa . . . pata pesa kidogo mikononi mwake! Uh-huh.

199 Ninashangaa ikiwa hiyo inaweza kutumika kwa Pentekoste? Tulipotoka kwenye kona ya barabara, na nje ya misheni ndogo kwenye uchochoro, na kisha tukapata kuwa na pesa kidogo. Na nashangaa ikiwa matembezi yetu hayajapotoshwa kidogo. Tulipopata kikundi cha . . . Labda kundi la watu huingia hapo, wanasema, “Loo, sawa, *hii*,” kuzungumza juu ya wanachama. Leo, yote mnayotaka ni wanachama, wanachama.

200 Mungu haangalii washiriki. Yeye anatafuta tabia, kwamba Yeye anaweza kuweka Neno Lake ndani ya mtu ambaye atamwamini Yeye. Kama nilivyosema, majuzi usiku, Eliezeri alitoa jasho hadi alipopata tabia ya bibi harusi. Halafu ilimbidi amfanye kusimama imara, ili aweze kuvikwa vizuri, kukutana na yule ambaye walikuwa wakizungumzia. Unaona? Kwa nini, ukipata tabia, huwezi kuwafanya wavalie vizuri. Hawawezi. Uh-huh. Sawa.

201 Angalia sasa, Pentekoste ya kisasa. Sasa, sasa, tumezungumza na Mpresbiteri, Mkatoliki, lakini nitazungumza juu ya Wapentekoste sasa, kwa sababu tunakwenda hapa kuwakilisha kitu. Unaona? Pentekoste, si ni jambo geni, kwamba, Wapentekoste katika wakati huu wa kisasa kwamba Biblia inatabiri watakuwa kama Laodikia? Laodikia. Kuna mwalimu wa Kigiriki ameketi hapa, ananisikiliza. *Laodikia* inamaanisha “mwanamke.” Laodikia ni jina la mwanamke, katika Kiyunani. Hakuna lolote la hayo mengine ya kanisa

linalowakilishwa na jina hilo. Lakini sasa ni mwanamke, Yezebeli. Hiyo ni kweli. "Na tukatajirika. Hatuna haja na chochote." Lakini hatujui kwamba sisi ni "uchi, vipofu, wenye mashaka," tukatoka nje ya Njia. Tumefanya nini? Tulichukua hazina kadhaa, labda, kama Yuda alivyofanya, unaona, basi hatukutembea nayo tena. Imeuzwa, kwa faida ya kibinafsi, watu wengi sana hufanya hivyo. Madhehebu mengi sana hupatana juu ya Neno, ili kupata washiriki wengi, faida ya kibinafsi; fanya chochote.

202 Hebu mchungaji fulani aingie katika jamii na ajenge kazi nzuri. Halafu wana mkutano, mkutano mkuu mahali fulani, ndipo wanamtoa mtu huyo nje, na kuchukua Ricky kipenzi kidogo na kumwingiza mle, na hiyo hutawanya kondoo tu. Kama Mungu akiweka mtu ndani. . . Lakini, loo, wanafanya hivyo kwenye mikutano, mara nyingi; wanachagua, kumfanya ndugu fulani maskini aondoke, na ambaye ameiendeleza kazi kwelikweli. Halafu, hawajui wanavunja shingo yao wenyewe kwa kufanya hivyo, na kuumiza kanisa.

203 Inauzwa, kwa umaarufu, maoni ya kibinafsi, faida, faida ya kibinafsi, makanisa makubwa, madhehebu makubwa. "Kundi letu ni kubwa kuliko yenu yote." Loo, hiyo ndiyo njia. Wabaptisti walikuwa na tamshi, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44." Lakini mmepata nini?

204 Nilisema, hivi majuzi usiku, "Maungamo; mawe ni maungamo." Jiwe lina uzuri gani bila mwashi wa jiwe aliye na Upanga mkali wa Mungu wenye makali kuwili, kuyatengeneza na kuyakata kuwa wana na binti za Mungu? Naam.

205 Yuda alifanya nini? Alifanya nini? Kumbuka hali yake ya mwisho. Loo, alifanya nini? Alitilia shaka madai ya Kristo, baada ya kuanza kutembea na Yeye. Wapentekoste, msifanye hivyo kamwe. Wafanyabiashara, msifanye hivyo kamwe. Msitilie shaka madai Yake. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Yuda alitilia shaka madai Yake, na akawa maarufu sana na akaiuza. Tabia ya Yuda ilimfanya amuuze, kwa wakosoaji Wake.

206 Na leo hii jambo lilo hilo linafanyika. Mara nyingi tabia ambayo tunajiruhusu tuumbike kwayo, hutuuza, kwa mahangaiko ya ulimwengu, kwa watu ambao wangekosoa. Kitu chenyewe ambacho Pentekoste ilitoka ndani yake, inarudi moja kwa moja ndani yake tena, wa kilimwengu tu karibu kama walivyokuwa mahali pa kwanza. Unaona? Ni nini hiyo? Tunakosa kuruhusu Uhai Wake kujiakisi ndani yetu.

207 Au, unajikuta ukitambulishwa na wanafunzi Wake wa kweli? Amina. Hapo ndipo tunataka kuwa, wa kweli Kwake, wa kweli kwa Neno Lake. Tukikaa imara, mbele ya wakosoaji! Amina. Je, hapo ndipo unapojikuta umetambulishwa usiku wa leo? Mshukuru Bwana. Amina. Kuruhusu Uzima wa Kristo kupitia kwao! Naam, bwana. Walikuwa wametakaswa na kuja

Kwake. Na mtu mwenye dhambi, katika kukiri . . . Na utakaso ulikuwa umewasafisha, na mioyo yao ilikuwa imemlenga Mungu hata Kristo alipojimimina Mwenyewe ndani yao na kuakisi Uwepo Wake kwa ulimwengu. Mbele ya wakosoaji, walisimama kama alivyofanya Yeye. Walisimama wa kweli kwa Neno, mpaka hata mmoja akasema, "Karibu unanishawishi kuwa Mkristo," mmoja wa nanii wake . . . wakosoaji.

208 Je, unaweza kujitambulisha na Petro kwenye Siku ya Pentekoste? Unaweza kujitambulisha hapo katika Matendo 2?

209 Ambapo, watu wanasema, leo, "Roho Mtakatifu alipewa mitume kumi na wawili tu."

210 Je, unaweza kujitambulisha na Petro, aliposema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na wale walio mbali, hata wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita"? Roho Mtakatifu yuyu huyu!

211 Je, unajitambulisha hapo pamoja naye siku hiyo? "Ninasimama nawe, Petro. Naam, bwana. Juu ya mafundisho yako ya kimsingi ya Maandiko, ninasimama hapo. Ninataka maisha yangu yaakisi Maandiko, kama tu vile yako yalivyofanya pale, wakati elfu tatu walipochomwa mioyoni mwao."

212 Walipoona ujasiri wao, siku chache baada ya hapo, walijua walikuwa pamoja na Yesu. Walikuwa na Neno, na wanajua Neno lilikuwa likiishi kupitia kwao. Nao waliogopa kuchezea Neno la Mungu, kwa sababu walikuwa mwakilishi wa Neno hilo, wakiwa na maisha ya namna hiyo, hata Mungu angejidhihirisha Mwenyewe moja kwa moja kuyapitia.

213 Alimwambia mtu, "Sina fedha na dhahabu. Sina majengo makubwa na mambo makubwa makubwa. Kile nilicho nacho, nitakupa. Katika Jina la Yesu Kristo, simama kwa miguu yako." "Kile nilicho nacho mimi!" Ilibidi awe na kitu kabla ya kuweza kumpa. Amina. Loo, jamani!

214 Tukiona kwamba Neno ni lile lile milele na milele, kila kizazi, wote ambao Mungu anaita wataona uakisi.

215 Au, pamoja na Paulo, wakati Dema maarufu, aliyependa ulimwengu alipomwacha, kwa ndugu zake Wakristo, wanavyojiita, wa maoni maarufu. Wakati Paulo alisimama juu ya Neno, "Dema alimwacha, upendo . . . akiupenda ulimwengu huu wa sasa." Akamwacha, kwa sababu alikuwa mkweli kwa Neno. Lilikuwa nyofu kupindukia kwake. Ungeenda na nani, Dema, au ungeenda na Paulo? Angalia Neno. Ungechukua upande gani katika hali yako ya sasa wakati huo? Hata hivyo, hao walikuwa wanaokiri kuwa Wakristo.

Paulo alisema, "Watu wote wameniacha." Maskini jamaa mdogo!

216 Siku zote nilikuwa nikimwogopa Dk. Ern Baxter. Alisema, "Unajua, nitakapofika Mbinguni, jambo la kwanza nitakalofanya?"

Nilisema, "Ni nini, Ndugu Ern?"

217 Akasema, "Nitatembea hadi kwa Dema na kumpiga kofi usoni kwa nguvu niwezavyo."

Nikasema, "Sasa, Ern."

218 Akasema, "Nitasema, 'Kwa nini ulimwacha Paulo huko chini namna hiyo?'"

219 Nikasema, "Unafikiri kweli atakuwa Huko, Ern?" Nilisema, "Kuwa mwangalifu kwa shauku yako ya kumpiga kofi usoni." Nikasema, "Nisingependa kuwa mahali alipokuwa, labda, unaona, lazima nifanye hivyo."

220 Kama vile yule kafiri alivyosema, alimwambia msichana huyo mdogo. Alisema, "Unaamini hiyo Biblia?"

Akasema, "Hakika."

221 Akasema, "Nadhani unaamini hadithi hiyo juu ya Yona, nyangumi kummeza Yona."

Akasema, "Hakika."

Akasema, "Utaithibitishaje, vinginevyo kwa imani?"

Akasema, "Nitakapofika Mbinguni, nitamuuliza Yona." Hiyo ni kweli.

Akasema, "Vipi ikiwa Yona hayuko Huko?"

222 Akasema, "Basi utamuuliza." Kwa hivyo nadhani hiyo inaitatua. Unaona? Naam, bwana. Ingembidi amwulize. Kwa hivyo, unaona, basi, hilo latosha.

223 Ninaamini, basi, ikiwa alimwacha Paulo na kuliacha Neno, alifanya jambo lile lile alilofanya Yuda. Naam, bwana. Ungechukua upande gani, mahali hapo? Sasa sikilizeni, Wapentekoste. Mngechukua upande gani? Nimekuwa nikiwachokora hawa Wapresbiteri, na kadhalika, sasa ungechukua nini? Ungechukua upande gani hapa?

224 Ama, hebu nikuulize jambo moja zaidi. Hili huenda likaumiza kidogo, lakini nataka kukuuliza jambo. Wakati, suala lilipoinuka katika kanisa la Korintho, kuhusu wahubiri wanawake; nao wakinyoa nywele zao, wanawake. Na suala likatokea, na Paulo akachukua msimamo, kwamba, "Hawapaswi kufanywa wahubiri." Paulo alichukua msimamo, kwamba, "Mwanamke, akikata nywele zake, amemdharau mumewe, na hafai hata kuonekana akisali hadharani." Je, katika hali yako ya sasa, ungechukua swala gani? Sasa angalia kwenye kioo. Afadhali niachane na hilo. Nataka uangalie hali yako ya sasa. Ni sehemu gani ambayo . . . Nini, wapi? Nini, wapi? Unaangalia wapi sasa? Unaangalia nini?

225 Paulo alikuwa akimwakisi Kristo. Je, unaamini hilo? Hakika.

226 "Paulo," unasema, "loo," mwanamke aliniambia, akasema, "alikuwa tu maskini mchukia-wanawake."

227 Paulo alisema, na—na huko katika Wagalatia 1:8, "Ikiwa Malaika kutoka Mbinguni akija na kuhubiri kitu kingine chochote isipokuwa hiki, kwenu, na alaaniwe." Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sasa, ni nini . . .

228 Unaakisi wapi sasa? Uh-huh. Usichukue upande maarufu. Chukua upande wa Neno. Uh-huh. Loo! Naam, bwana. "Alimwacha."

Na wakati suala lilipoibuka, mbona, Paulo alichukua msimamo.

Nao waliandika, wakasema, "Roho Mtakatifu alituambia tufanye hivyo."

229 Akasema, "Nini? Neno la Mungu lilitoka kwako, au lilitoka kwako peke yako? Mtu yeyote akijiona kuwa wa kiroho au—au nabii, atakubali kwamba vitu ninavyoandika ni amri za Bwana." Ilikuwa ni nini? Alikuwa akidumu na Neno. Amina.

230 Sasa, unakaa wapi? Hiyo ni juu yako sasa. Wewe tafuta tu mahali pako. Vema. Naam, bwana.

231 Hapo Paulo alisimama, kwa—kwa . . . kutoka kwa nafasi aliyokuwa nayo. Kumbuka, Paulo, kufanya hivi . . . Sasa, subiri. Hebu nitoe kitu kingine kabla hatujaondoka. Paulo, kabla ya kufanya hivi, ilimbidi aache cheo cha juu alichokuwa nacho katika kanisa la siku zake, ili kudumu na Neno.

232 Sasa, ikiwa unamwangalia Paulo, na wewe je, wakati kanisa lako linafundisha kinyume na Hilo? Na wewe je, mchungaji, mhudumu, walei? Hakika.

233 Alifanya nini? Ilimbidi achukue msimamo huu ili Mbegu hii ikue, Mbegu ya Uzima wa Milele. Hakuwa kinyume. Alisema, "Hata ni hivyo, sheria inasema." Hiyo ni kweli. Hakuwa . . . Alikaa sawa na Neno. Na kufanya hivyo, ilimbidi aache kanisa lake la kawaida, kuifanya. Ili kudumisha Neno la Uzima likikua, ilibidi afanye hivi.

234 Dema na wengine wote, walisema, "Loo, unaweza pia kuja. Endelea, Paulo, wewe sio . . . "

235 Lakini Paulo alisimama pale pale na Neno hilo. Yule maskini, Myahudi mdogo mwenye pua iliyojipinda, mimi nataka kumwona Siku hiyo. Ninataka kusimama pale, nimwone akivaa hiyo taji ya mfia imani wakati atakapojitokeza. Nataka kuona hapo, na kusema, "Utukufu! Haleluya! Paulo!" Amina. Naam, bwana. "Dumu kwenye Neno! Nina furaha, Paulo." Kwa hivyo, nisaidie, Mungu. Hebu nikae mahali pale pale. Naam, bwana. Naam.

236 Katika ono ambalo nililiona si muda mrefu uliopita, la hao watu kule juu, niliuliza swali. Uliisoma katika mu—muhtasari, makala ya Wafanyabiashara. Walisema . . . Vema, nikasema, "Inambidi Paulo?"

Kasema, "Naam, bwana."

237 Nikasema, "Nilisimama juu ya Jambo lile lile alilosimamia." Naam, bwana. Dumu, jambo lile lile.

238 Musa ilimbidi ainame kutoka kwenye kiti cha enzi, kuchukua Neno la Mungu. Aliacha kiti cha enzi. Hiyo ni kweli. Alikuwa mrithi wa kiti cha enzi. "Na akaacha raha za kuwa Farao, kwani alihesabu aibu ya Kristo kuwa utajiri mkubwa kuliko hazina za Misri."

239 Unasema, "Vema, nakwambia. Wanawake wote watanicheka. Wanaume watafikiria . . . " Sijali wanafikiria nini. Hiyo ni kweli.

240 Paulo aliinama. Musa aliinama kutoka kwenye kiti cha enzi. Nina mlolongo wao umeandikwa hapa, umechukua kurasa tatu. Lakini hebu niwaambieni jambo, niwasaidie, haraka sana.

241 Yesu aliinama kutoka Mbinguni, kujidhihirisha Mwenyewe katika umbo la mwili wenye dhambi. (Na wewe ni nani, au mimi ni nani?) Kufanya . . . atutengenezee njia ya kumwakisi Mungu, kutengeneza njia ya kujiakisi Mwenyewe ndani yetu, kwa kututakasa kwa Neno Lake. Kwa maana Neno Lake linasema, kwamba, wakati Yeye alifanya hivyo, ili tuweze kuakisi Neno Lake.

242 Katika Yohana 14:12, Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi atazifanya pia." Kwa nini? Ilikuwa ni Kristo, akiakisi. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena. Hata hivyo, nyinyi mtaniona, kwa kuwa Mimi . . . " ("Mimi," kiwakilishi cha nafsi.) " . . . kuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, unaona, yote hadi mwisho wa ulimwengu." Loo!

243 "Ikiwa yeyote atanifuata, na ajikane mwenyewe. Acha akane imani yake iliyobuniwa na wanadamu, achukue Biblia yake na kunifuata." Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

244 Halafu, unatambulishwa mahali fulani katika Maandiko. Bila shaka, itanibidi kufunga. Unatambulishwa mahali fulani katika Maandiko. Unajua hilo. Kila mmoja wetu, tunaona utambulisho wetu.

245 Kanisa, tunakwenda hapa kwenye—kwenye mkutano ambao umepangwa kwa mwaka. Makanisa yamekuwa yakiomba. Watu wamekuwa wakifunga. Nimemwaga moyo wangu, kote katika wiki hii, huku na huku kwenye bonde hili, kwa kila ufa na kona ndogo ambayo ningeweza kuingia, nikijaribu kadiri niwezavyo kukuonyeni juu ya Kuja kwa Bwana. Na sisi hapa, kabla tu ya

wakati huu hapa. Na hebu tujitambulishe sasa, tuvuke kule, kuwakilisha, au kumwakisi Yesu Kristo.

246 Je, tutajitambulisha na mtindo mpya wa kukata nywele? Je, tutajitambulisha na jinsi tunavyoweza kuvalia? Je, tutajitambulisha jinsi tunavyoweza kusimama na kuongea kwa umaarufu, kiasi cha elimu tuliyo nayo? Wakati, Paulo alisema, "Mambo hayo, ilimbidi kuyasahau, ili amjue Kristo."

247 Je, tunatambulisha pentekoste? Je, tunatambulisha? Ni nini, ni wapi tunajikuta tukiakisi?

248 Tunaakisi nini, hata hivyo, ikiwa tu tuna kelele nyingi, na tunaweza kupiga kelele na kucheza, na kuruka juu-na-chini? Loo, nimeona Waislamu wakifanya hivyo. Nimeona nyani wakifanya hivyo.

249 Hakuna maoni. Simaanishi hayo, kutania. *Hapa* sio mahali pa utani. Hili ni Neno la Mungu. Unaona?

250 Lakini nimeona wanyama wakiruka, wakicheza, sungura. Hiyo haimaanishi chochote. Hakika sivyo. Una furaha. Chochote kinaweza kukufurahisha, kutazama juu kidogo. Nimewaona wenye dhambi wakiwa wamelewa sana, na wenye furaha sana! Hakika. Hiyo haimaanishi kitu.

251 Lakini furaha hiyo inatoka wapi? Rasilimali ni nini? Je, inaathiri nini kwako? Inaakisi nini juu yako? Mtu atakana Neno la Mungu; mtu ataishi ulimwenguni; mtu atasikia Ukweli na kuuondokea; wauze haki zao za kuzaliwa, kwa ajili ya kitu kingine?

252 Loo, Mungu atusaidie, ndugu, dada, tusaidie kurudi na kumruhusu Kristo ajiakisi Mwenyewe, pia, ndani yetu, namna hiyo. Loo, jamani! Mungu na atusaidie kutambulishwa ndani Yake, sana, hata Neno Lake na Uwepo Wake uweze kutiririka kupitia sisi, kujidhihirisha Mwenyewe kwa ulimwengu, amina, ambayo tutakabiliana nayo.

253 Tamshi moja zaidi, ninafunga. Sikiliza kwa makini. Mhunzi wa dhahabu sasa amesimama tayari.

254 Unajua, vito vinapatikana duniani, vifaa ambavyo tunapiga pamoja. Lakini, unajua, ikiwa utapata ndani ya hiyo, kitu kilichochanganywa ndani yake, hicho kibamba ulicho nacho kitavunjika. Mnyororo hauna nguvu zaidi kuliko kiungo chake kilicho dhaifu sana.

255 Kwa hivyo, ikiwa unajaribu kuwa jiwe lililokatwa kutoka kwa Mungu, nyenzo zingine, na unaona unajaribu kujifanya mkubwa sana, na katikati hapo ulilazimika kupenyeza ulimwengu kidogo ndani yake, jiwe hilo litavunjika. Halitastahimili jaribio. Basi, sikilizeni, Mungu hatatukubali, watu wa Pentekoste, tunapoingiza kanuni na kila kitu kingine katika Neno la Mungu. Itakuwa. . .Mungu atalikataa jiwe na kulipiga teke upande mmoja. Hebu tusitafute vitu vikubwa.

Wacha tumtafute Kristo maishani mwetu. Tutafute unyenyekevu. Unaona?

256 Kumbuka, ikiwa jiwe ni kubwa, na unajaribu kuenea, hicho ndicho ninaogopa tunajaribu kufanya. Hayo ndiyo mazungumzo niliyo nayo na hawa Wafanyabiashara. Inaonekana kama wanazidi kitu fulani. Na mimi—mimi. . .Hiyo ndiyo sababu nachukia. . .Mimi—mimi—mimi ninapenda kuwa mkweli kwenu, ndugu. Nitakutana nawe kule katika Hukumu siku moja. Hiyo ndiyo sababu kanisa linadhani mimi niko kinyume na kanisa. Sipingi kanisa. Mimi. . .

257 Kwa nini nijitambulishe hapa pamoja nanyi? Ikiwa nilidhani Mbaptisti alikuwa sahihi, Mmethodisti alikuwa sahihi, Mpresbiteri alikuwa sahihi, ningekuwa pamoja nao. Nipo hapa pamoja nanyi kwa sababu ninajitambulisha hapa na nyinyi.

258 Lakini msijaribu kupita mipaka yenu sasa, kuwa kitu usicho. Usijaribu kujifanya mkubwa, kujilinganisha na mtu mwingine, na kuingiza ulimwengu hapo ndani, kupata washiriki zaidi na kadhalika. Kitu hicho kitavunjika mara mbili, na Mungu atakitupa ndani ya chungu kule, ili kifinyangwe upya.

259 Atainua watoto kutoka kwenye mawe haya mengine, kwa Ibrahimu. Hiyo ni kweli. Atafanya hivyo. Atachukua Mpresbiteri, alete kitu kutoka kwake; Methodisti, au Wabaptisti. Na inaonekana kama ameanza hivyo.

260 Je, mnanisikia, Wafanyabiashara? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa sababu tu tuna jina la "Pentekoste," hiyo haina maana kwa Mungu. La, bwana.

261 Pentekoste si shirika. Pentekoste ni tukio. Ni uakisi wa Kristo, ambapo alianza kwenye Siku ya Pentekoste, kujiakisi Mwenyewe kupitia watu.

262 Halafu watu wanaanza kuongeza ulimwengu. Nini kilitokea? Waliingia katika Baraza la Nikea, na—na kukataa ahadi zilizo wazi za Mungu, na kuweka mafundisho ya sharti ndani yake. Na akavunja uzoefu wa Kikristo vipande vipande, na kuingia katika Ukatoliki.

263 Luther alianzisha matengenezo. Na yeye akadhihirisha, na ikavunja kitu hicho tena.

264 Wamethodisti walikuja na utakaso. Na akaanza kujitokeza, naye akafanya vivyo hivyo.

265 Na Wapentekoste wanafanya jambo lile lile. Loo! Vema, unaiangalia, unaweza kuiona.

266 "Unafanyaje wewe," unasema, "unajuaje mambo hayo?" Vema, hebu nikuambie kitu.

"Ndugu Branham, unatabiri?"

267 Sitabiri hasa. Lakini wakati daktari anamchunguza mgonjwa, anaona dalili, anajua ni nini kitakachofanyika.

Nasoma kutoka kwenye Kitabu cha Daktari. Na ninaona dalili zinafanya kazi katika kanisa la Pentekoste, na ninajua linakoelelekea.

268 Likomesheni. Acheni. Rudini. Mungu awasaidie. Msiende hivyo, enyi watu. Hivi hamwezi kuona kile ninachojaribu kufanya? Ninachoma moto maisha yangu, kujaribu kukuokoa kutoka kwa kitu hiki kichaa unachokimbilia. Siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, mimi hupaza sauti kabisa. Nanyi mnafikiri mimi ni adui yenu. Mimi ni ndugu yenu. Rudini. Msiende hivyo. Hivi hamuoni kile kilichotokea wakati wengine walikwenda hivyo?

269 Wafanyabiashara, kaeni mbali na njia hiyo. Sasa mnaandika kila aina ya kanuni za imani kwenye majarida yenu, na hiyo inawashirikisha na dhehebu kama tu wengine wote. Mnajua hivyo tu ndivyo ilivyo. Hamwoni? Mnaingia moja kwa moja katika jambo ambalo mmekuwa mkipinga. Sasa, hamtanipenda, labda. Milele, hiyo ni kweli. Andikeni neno langu. Geukeni, la sivyo mmekwisha.

270 Pentekoste, geukeni, la sivyo mmekwisha. Rudini kwenye Neno. Muda umeenda kuliko mnavyodhania.

271 Mungu anataka kuakisi, sio washiriki, lakini mawe halisi ambayo yamepigwa msasa na kufinyangwa na kuchongwa. Tazama. Mfua Dhahabu amesimama usiku wa leo, tayari kutoa mashaka yote ya taka, yote yaliyo dhidi yenu. Na kwa . . . Yupo hapa, tayari kuwafinyanga na kuwachonga muwe waaminio, akiondoa mashaka yote kutoka kwenu.

272 Nyinyi endeleeni, mmeona waigaji wengi wakija, wakisema, "*Hii*, na, utukufu kwa Mungu, nimepata *hii*. Na, haleluya, nimepata *hii*." Na unakuta, hawajapata chochote. Na shetani alifanya hivyo, ili kuzua shaka moyoni mwako. Unaona? Alifanya hivyo, makusudi, kufanya hivyo. Lakini kumbuka, hiyo inasema jambo moja tu, kwamba, kuna hiyo iliyo halisi ambayo mwigaji huyo anajaribu kuiga.

273 Kuna Roho Mtakatifu halisi. Kuna Roho halisi wa Mungu. Kuna nguvu halisi za Mungu. Kuna Mwana wa Mungu anayejidhihirisha Mwenyewe usiku wa leo kama Roho Mtakatifu, kuonyesha Maisha Yake. Amesimama hapa usiku wa leo katikati yenu, katika umbo la Roho Mtakatifu; kupiga taka zote zitoke kwako, mashaka; na kukuonyesha wewe, ufufuo Wake, kwamba hajafa. Naye yupo hapa kukuonyesha ya kwamba Yeye anaishi, yeye yule jana, leo, na hata milele. Yupo hapa kujitambulisha Mwenyewe pamoja na sisi. Je, haitupasi basi kujitambulisha na Yeye, kuamini Neno Lake na kulichukua?

274 Na tuombe.

[Ndugu mmoja anatabiri—Mh.] Utukufu. Amina. Amina. Loo! Amina.

275 Ee Bwana Mungu, jinsi tunavyokushukuru Wewe, Bwana! Tunaambiwa katika Maandiko, kwamba wakati Daudi, wakati adui alikuwa anaingia, nao wakakusanyika pamoja, naye Daudi alikuwa akijaribu kuwaambia kuhusu Mungu, alisimama mmoja katikati yao, akatabiri na kuwaambia cha kufanya, na jinsi ya kumshinda adui. Kwa kweli, Bwana, tunaamini jambo lilo hilo, Roho wa Mungu hushuka miongoni mwetu, na Neno ndilo mahali pa kumshinda adui.

276 Hicho ndicho ulichowapa Adamu na Hawa, katika bustani ya Edeni, kumshinda adui. Na wakati Hawa alihojiana na Hilo, na akaleta hoja kwenye Neno, lilianguka, na dhambi ikaingia.

277 Kwa kweli, Bwana, hilo limekuwa anguko la wanadamu, kote katika nyakati zote, kujaribu kuingiza kitu pamoja na Neno. Sara alijaribu jambo lile lile, kuingiza kitu fulani, kumwingiza Hajiri, kumleta mtoto, lakini likaanguka. Daima, imekuwa hivyo, Baba. Sisi—sisi tunataka tu Neno Lako, na hilo peke yake; bila chochote kuongezewa Kwake, au kuondolewa Kwake, jinsi tu lilivyo. Na Wewe ndiwe Neno hili. Nasi tunashukuru kwa hilo.

278 Wabariki watu hapa, Bwana. Mimi sasa, katika hizi, usiku baada ya usiku, nimejaribu kusema mambo haya, kwamba Ku—Ku—Kuja Kwako kumekaribia. Kila kitu kinaumbika kwa njia hiyo.

279 Na kutoka kwenye o—ono, majuma machache yaliyopita, amenituma hapa Arizona. Sijui kwa nini. Labda ni kuja kwangu Nyumbani. Sijui. I—inaonekana sana hivyo.

280 Lakini, Bwana, acha nimalize mwendo wangu na...na kushikilia Imani, kuweka mavazi yangu bila doa, Bwana, kwa neema ya Kristo. Jalia niweze kusimama katika siku hiyo, na kusema, "Nimetangaza Shauri lote la Mungu, kama nilivyolijua kuwa ni Kweli, na sikuepuka kusema chochote." Tujalie.

281 Wajalie ndugu zangu, Bwana, vivyo hivyo, waungane pamoja na kusogea karibu zaidi, na kujua kwamba mawaidha haya si—si kemeo, lakini ni onyo, na kuangalia njia panda. Tujalie, Baba. Kama tulivyoambiwa tu, kwamba, Yeye angetuhukumu kwa Neno hilo la Ujumbe. Mungu, jalia nijiangalie mwenyewe, na, ninaionea aibu, Bwana, kwenye kioo cha Neno la Mungu.

282 Ninagombea, "Na kwa uaminifu, tukipigania kwa bidii Imani ambayo walipewa watakatifu mara moja," kama vile Yuda alisema tunapaswa kufanya. Na tumeahidiwa, kwamba, "Katika siku za mwisho, Imani hii ya baba ingerejeshwa tena, kwenye Imani ya asili ya kipentekoste." Uliahidi hiyo, katika Malaki 4. Ulisema kwamba itatokea. Pia, Baba, jalia tuwe macho, na ma—macho yetu yakiwa wazi, na tusiikose, kama vile kwenye nyakati ambazo wamekuwa wakifanya kila wakati. Lakini macho yetu na yafunguke, kumwona Yesu Kristo vile Yeye amejidhihirisha katika utukufu Wake kati ya watu Wake

wanyenyekevu, kuchukua watu, kutoka kwa hawa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake. Ijalie, Bwana.

283 Bariki kusanyiko hili sasa. Nimezungumza kirefu. Bwana, siwezi kuomba msamaha (kwa sababu, nilihisi kusema niliyosema), kwa kuwashikilia kwa muda mrefu. Lakini ninakushukuru kwa ajili ya wanaume na wanawake, leo hii, ambao wa—wanaweza kusimama, na watapinduka, na—na kujaribu kushikilia mi—miguu yao sakafuni, na kusikiliza Ujumbe. Ninakushukuru Wewe kwa ajili ya makanisa kama haya, ambayo yatafungua mlango na kusema, "Njoo ndani. Tufundishe. Au, hubiri na sisi. Tusaidie." Mungu, asante kwa haya.

284 Na asante kwa mahali pa jangwani palipo na rutuba na maji, pia, kwa ulimwengu wa biashara, hawa Wafanyabiashara. Bwana, nguo zao zikae bila doa kutoka kwa vitu vya ulimwengu. Tujalie. Pafanye mahali pa kuokolea nafsi, Bwana, ambapo—ambapo labda, mahali fulani watu hawataenda kanisani, wataenda kusikia wafanyabiashara wakiongea. Na hebu ma—maisha yao yakolee chumvi na neema ya Mungu sana, na unyenyekevu wa Roho Wake, hata—hata ulimwengu utatamani kuwa aina hiyo ya watu. Tujalie, Bwana. Utubariki sasa, pamoja.

285 Bwana, utusamehe mapungufu yetu. Tusamehe dhambi zetu, na ujalie mifereji ya mioyo yetu kufunguka. Mfalme wa Utukufu na aingie kati yetu sasa, ikiwa tumepata neema machoni Pako, kwa kutubu makosa yetu. Bila shaka, moyo wangu umetubu, mioyo mingine mingi imetubu. Na ikiwa tumepata neema, Bwana. Tufinyange sasa.

286 Safisha mahekalu yetu, ili Neno la Mungu aliye hai liishi kati yetu na kuthibitisha kwamba Yesu Kristo hajafa. Yeye sio mwanzilishi aliyekufa kama Muhammad, au—au Buddha, au dini zingine potovu. Yeye ni wakati ulio hai, uliopo sasa, Yesu aliyefufuka. "Yeye yu hai milele na milele, na hawezi kufa tena," na ametupa Uzima wa Milele, na amejiwasilisha Mwenyewe miongoni mwetu. Na sisi, Bwana, tunaonyesha neema Yake kwa wengine.

287 Tusaidie, Baba, kama ulivyoahidi katika siku za mwisho kile kitakachotokea, kama tu ilivyokuwa katika siku za Lutu. Tujalie sisi, kama wale waliokuja kutoka Emau, tuende nyumbani usiku wa leo, tukishangilia, kwa sababu tunakuona ukifanya jambo kama vile walivyokuona ukifanya baada ya kufufuka Kwako kutoka kwa wafu; wakijua ilikuwa ni jambo lile lile ulilofanya Wewe kabla hujafa, ndipo walijua ya kwamba ulikuwa umefufuka. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

288 Sasa, sasa, ni—nimezungumza kwa kirefu. Lakini, hii, sijui kwamba Yeye angefanya hivi. Sijui kwamba Yeye atafanya.

Nitamwomba tu. Ninaamini, ikiwa nitaweka maisha yangu hapa ili. . .kwenye nguzo, kusimama na Neno hili, basi, kadiri ya ufahamu wangu.

289 Si kwamba sina dhambi. Nina nyingi zikining'inia juu yangu. Lakini, kila saa mimi hukiri, kila wakati. Wakati ninapoona makosa yangu, basi mimi huacha hayo, na kujaribu kufanya yaliyo sahihi. Nisingejaribu kwenda Mbinguni kwa sifa zangu. Nisingefika huko. Ninamtumainia Yesu Kristo kwa dhati. Yeye ndiye Tumaini langu. Na—na—namwamini. Nisingejaribu kuingia kwa sababu mimi ni ndugu wa Pentekoste. Ni—nisingeingia juu ya sifa za Pentekoste. Ninaingia juu ya sifa za Damu ya Yesu Kristo. Alikufa kwa ajili yangu.

290 Na hiyo ndiyo ninayotaka utumainie, sifa Zake. Halafu basi unajuaje unafika huko? Ni wakati, kila Neno, unapoliitikia Hilo kwa "amina, amina." Kwa sababu, Hilo ni Neno Lenyewe linajaribu kujithibitisha Lenyewe. Na tukilikana Neno hilo, linawezaje kujithibitisha Lenyewe?

291 Sasa, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Hiyo ni kweli? Halafu alisema nini katika Yohana 5:19? "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya chochote kwa nafsi Yake, ila kile anachomwona Baba akifanya."

292 Alipita kwenye birika la Bethesda. Hapo palikuwa na umati wa watu, labda mara ishirini au thelathini ya ule ulio ndani ya jengo hili usiku wa leo. Kuna watu mia nne au mia tano, labda, wanaoketi hapa usiku wa leo. Sijui, lakini kunaweza kuwa na wengi hivyo. Lakini labda kuna maelfu. Ninafahamu kuwa "umati" ungekuwa maelfu. Sasa, akiwa amelala pale, pamoja na vilema, viwete, vipofu, na waliopooza, Yeye alimponya mtu mmoja, kwa sababu alijua kuwa mtu huyo amekuwa hivyo. Baba alikuwa amemwonyesha. Unaona? Aliwaacha wengine. Unaona? Ndipo akaulizwa hivyo.

293 Lakini Biblia ilisema, baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, kwamba, usiku wa leo, "Yeye ni Kuhani Mkuu." Je, mnaamini hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je, mnaamini Yeye angali hai. ["Amina."] Na Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na hisia za udhaifu wetu? ["Amina."] Vema, ikiwa Yeye ndiye Kuhani Mkuu yule yule, kulingana na Waebrania 13: 8, basi angefanya vile vile. Hiyo ni kweli?

294 Sasa na tuisafishe mioyo yetu kutoka kwa dhambi zote. Naomba tukiri makosa yetu. Na tukiri kutokuamini kwetu, kwamba tumekosea, na kusema, "Bwana Yesu, mimi hapa. Ninahitaji, usiku wa leo. Jiakisi Mwenyewe katika maisha yangu. Nipe imani aliyokuwa nayo yule mwanamke, aliyegusa vazi Lako."

295 Nami nitasema, "Bwana Yesu, nimesimama na Neno Lako." Hiyo ndiyo ilikuwa agizo langu, "Lihubiri Neno." Nimesimama

Nalo. Na—nataka kufa Nalo. Nami nime—nimesimama na kutengeneza vitu vigumu, kwa sababu ya Neno, na kukaa hapo, lakini Yeye daima amelithibitisha Hilo.

296 Sasa ninamtegemea Yeye athibitishe Neno hilo. Acha itupe. . .Hebu Yeye atirike kupitia sisi usiku wa leo, tunapoomba.

297 Ni wangapi hapa ndani walio wagonjwa, wahitaji, walio na haja ya kitu chochote? Inua mikono yako na kusema, "Ni mimi, Bwana. Naamini, Bwana."

298 Nataka usikivu wenu usiogawanyika, kwa utamu kadiri mwezavyo, kwa muda mfupi.

299 Ikiwa, baada ya Ujumbe huu, na Kristo atajiakisi Mwenyewe ndani ya watu, na uone kwamba mtu maskini ana imani ya kutosha kugusa vazi Lake, nami ninaweza kujisalimisha kwa Roho Wake, na kujua kwamba huyu ni Roho Mtakatifu! Basi, ikiwa wewe ni wa kitu kingine isipokuwa kikundi kinachoamini Hili, basi ningefika mahali wanaamini Ukweli. Unaona? Ningefika. Kwa kweli ningefika. Ningeamini, kwa sababu Mungu anajitambulisha Mwenyewe. Usijitambulishe sasa na Mafarisayo na wale ambao hawaamini, hao vipofu, kwa sababu Yesu alisema hawatamwona tena. "Lakini mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi. Nitakuwa ndani yenu. Mtaniona Mimi." Vema, ikiwa Yeye ndiye Kuhani Mkuu yule yule, hivyo ndivyo ungemwona, kwa kujidhihirisha Mwenyewe kwa njia ile ile aliyoifanya wakati huo. Hiyo ni kweli? Vema.

300 Sasa, amini kwa moyo wako wote. Kuwa na imani. Usitie shaka, ukiomba, na kisha tuta—tutaona kile alichosema. Sasa, amini tu kwa moyo wako wote.

301 Sasa, Baba Mungu, nimezungumza juu Yako na kwa ajili ya Neno Lako. Nimefanya hivyo kwa njia iliyovunjika, Bwana, najua, lakini ndiyo njia bora zaidi nijuayo. Wiki hizi zote mbili, nimekaa Nayo kila wakati, Bwana. Maisha yangu yote, nimejaribu kukaa Nayo. Sasa, Bwana, liheshimu Neno Lako usiku wa leo hapa, wakati uamsho unapofunga. Acha ijulikane, Bwana, kwamba ikiwa tunasimama kwa kile kilicho sawa, haki itasimama kwa ajili yetu. Tujalie, Bwana. Kwamba tunaamini, kwamba Wewe unakuwa sisi, kuchukua dhambi yetu; ili tuweze kuwa Wewe, wana wa Mungu, kuakisi Neno la Mungu, lililothibitishwa, likadhihirishwa kupitia maisha yetu ya huduma ambayo Wewe umetupatia. Tujalie, Bwana. Tunajiwasilisha Kwako sasa katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

302 Sasa kuwa tu imani. Usiwe na shaka, bali—bali uamini kwa moyo wako wote sasa. Je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kila mtu amini. Sasa, usitie shaka. Omba tu, kimoyomoyo. Kuwa na imani sasa. Usitie shaka, hata kidogo. Jitulize sasa. Sikiliza kile Roho anachokuambia. Kuwa na imani katika Mungu. Kuwa na imani katika Mungu.

303 Mbona unaniangalia kwa unyofu namna hiyo? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Sikujui. Sijawahi kukuona, ila mwanamke tu aliyeketi hapo akiniangalia. Sio kabisa ugonjwa ambao ana wasiwasi juu yake. Ana wasiwasi juu ya mtu mwingine. Ni msichana mdogo. Amepotea tu. Ameondoka nyumbani. Yeye ni msichana tu, msichana tineja. Hii imetengenezwa kwa muda mrefu. Hadi sasa, sioni akiwa hatarini. Kuwa na imani. Mwamini Mungu, atamtuma nyumbani kwako.

304 Aligusa nini? Sasa, unamwona huyo mwanamke. Sijawahi kumuona maishani mwangu. Yeye, kabisa, ni mgeni.

305 Huyu hapa mwanamke ameketi nyuma *hapa*, macho yamefungwa, akiomba. Anasumbuliwa na shi—shida ya rektamu, na ni bawasiri. Anaugua ugonjwa wa moyo. Ataukosa. Mungu, tusaidie. Bi Willingham, mwamini Bwana Yesu Kristo. Sasa unaupokea.

306 Sasa muulizeni huyo mwanamke. Hatufahamiani kabisa. Unasema, "Uliita jina lake."

307 Kwa nini, hivi Yesu hakumwambia Simoni, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona." Kuwa tu na imani kwa Mungu. Je, unaiamini?

308 Sasa kuwa mnyoofu. Amini. Usitie shaka. Weka tu mawazo yako kwa Mungu, na—na umwamini Yeye.

309 Anafanya nini? Anajitambulisha Mwenyewe. Anajiakisi Mwenyewe. Sasa, ikiwa hufikirii kwamba ni sahihi, nakuomba uje kwenye mimbara na ufanye vivyo hivyo.

310 Kuna mwa—mwanamke mdogo. Ameketi hapa nyuma na shela juu ya kichwa chake. Yeye ni Mhispania. Naye anamwombea binti. Huyo binti haishi hapa. Sasa ameweka mikono yake usoni mwake. Naye ni . . . Binti huyu anaishi mahali ambapo pana maji mengi, ambapo bahari inanguruma, huko San Diego, California. Na ana mshipa uliovimba daima na matatizo, na yuko karibu kurukwa akili. Je, unaamini kwamba sala yako iligusa pindo la vazi Lake, maskini dada yangu Mhispania, na binti yako atapona? Kama unaamini, inua mkono wako na ukubali. Sawa, unaweza kuwa nao. Inageuka mwanga hapo karibu na wewe sasa. Usiwe na shaka. Amini.

311 Hiyo ilikuwa ya kushangaza kwako, sivyo, mama, uliyeketi hapo? Uliweka mkono wako puani mwako, na kupangusa uso wako wakati huo; ukasema kitu kupitia marefu ya kanisa; ukiwa umevaa koti la samawati, umeketi pale. Ndiyo. Sawa. Ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, basi moyo huo utanyooka na hutapata shida yoyote ya moyo ambayo umekuwa ukiteswa nayo. Ikiwa hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako, ili ushuhudie tu kwamba hiyo ni kweli. Mimi ni mgeni kwa huyo mama. Amina. Unaamini? Hakika. Uh-huh. Daima amini.

312 Naona, na badala yake ni mtu wa makamu. Je, unaona hiyo Nuru, kaharabu, inayoning'inia hapo hapo, ikivuta juu ya yule jamaa? Sasa anaomba. Ameinamisha kichwa chake. Na kuna jambo ambalo ndiyo kwanza lisemwe, ambalo lilivutia usikivu wake kuomba. Maana, ametoka California, pia, kama nilivyosema. Lakini ametoka Fresno, California. Anaugua pumu. Bw. Korol, ikiwa unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda nyumbani na kuwa mzima, pia. Amina. Amini sasa. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Je, hatufahamiani? Inua mkono wako. Vema.

313 Unaamini? Mtu huyo aligusa nini? Alimgusa Yesu Kristo. Yuko futi thelathini kutoka kwangu.

314 Ninakupa changamoto, katika Jina la Yesu Kristo, kuamini kwamba Ujumbe huu wa Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho ndio kufunga kwa historia ya ulimwengu. Ninakupa changamoto kuamini kwamba mimi—mimi nimekufundisha usiku wa leo. Amini kwamba Mungu amenituma. Iheshimu. Na sasa, usiniheshimu mimi, lakini heshimu kile Yeye alichonitumia, Neno Lake, na Mungu atakupa, haja yako. Siwezi kumfanya afanye hivyo, ila ikiwa utaamini.

315 Hapa, angalia hapa. Hivi huwezi kuona Hilo? Angalia hapa, hiyo Nuru papa *hapa*. Iko moja kwa moja juu ya mwanamke huyu mnene kiasi anayeketi hapa. Simjui mwanamke huyo. Sijawahi kumuona maishani mwangu, lakini yeye ni mgonjwa. Anateseka. Amekuwa kwa daktari, na, kitu fulani, uchunguzi ulionyesha uko kwenye koloni. Ni kitu kama vidonda. Hapana, daktari anasema ni vidonda kwenye koloni. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hutoki hapa. Uko hapa kwenye matembezi. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Unatoka Michigan. Hiyo ni kweli. Uko hapa kumtembelea mtoto wa kiume, naye yuko katika namna fulani ya biashara ya redio ya aina fulani. Unaitwa Bibi Erb. Kuwa na imani katika Mungu. Nenda nyumbani ukakute jinsi unavyoitaka wewe, ikiwa unaamini kwa moyo wako wote.

316 Unaamini? Je, uko tayari kuachilia takataka za kutokuamini zipigwe zitoke kwako? Je, unaamini kwamba unaweza kumwona Kristo akijidhihirisha Mwenyewe, yeye yule jana, leo, na hata milele? Yeye ni Mungu. Je, unaamini hilo? Sema, "Amina" ikiwa unaliamini. [Kusanyiko linasema,"Amina."—Mh.]

317 Basi wekeaneni mikono mmoja juu ya mwingine. Nitawaonyesha Neno Lake, ikiwa ninyi ni waaminio. Alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya." Wekeaneni mikono mmoja na mwenzake sasa.

318 Funga macho yako. Inamisha kichwa chako. Ombeaneni. Wewe omba. Sio mimi. Wewe omba. Kristo, nje kati yenu huko nje!

319 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, Kristo na aonekane katika kila maisha hapa usiku wa leo. Na uponye wagonjwa, Bwana. Tunamfukuza kila pepo wa kutokuamini, ili Kanisa la Pentekoste liweze kuona uakisi wa Yesu Kristo katika maisha yao, kama walivyouona usiku huu.

*UTAMBULISHO* SWA63-0123
(Identification)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 23 Januari, 1963, kwenye First Assembly Of God huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org